JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2025

Mei, 2026

TAARIFA YA HALI YA DAWA ZA KULEVYA YA MWAKA 2025

Imetayarishwa na
MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA,
S.L.P 80327,
8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam
Barua pepe : cg@dcea.go.tz
Tovuti : www.dcea.go.tz
Instagram : @dceatanzania
Twitter : @dceatanzania
Facebook : dcea_tz
YouTube : DCEATV
Simu ya bure: 119

ISBN:978-9912-9896-5-8

Imetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya mwaka 2015

YALIYOMO

MAELEZO YA WAZIRI vi
DIBAJI viii
FAHARASA ix

SURA YA KWANZA 1
HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI 1
1.1 Utangulizi 1
1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani 1
1.4 Heroin 4
1.5 Hali ya Biashara na Matumizi ya Cocaine Duniani 4
1.6 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya 5
1.7 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetanine Type Stimulants-ATS) 6
1.8 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS) 6
1.9 Jinsia na Matumizi ya Dawa za Kulevya 7
1.10 Dawa za Kulevya na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia 8
1.11 Matumizi ya Dawa za Kulevya miongoni mwa Wanafunzi 8

SURA YA PILI 10
MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI 10
2.1 Utangulizi 10
2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction) 10
2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction) 10
2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction) 11
2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa (National, Regional and International Cooperation) 11

SURA YA TATU 12

UDHIBITI WA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA (SUPPLY REDUCTION) 12

3.1 Utangulizi 12

3.2 Operesheni za Ukamataji wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2025 12

3.3 Raia wa Kigeni waliokamatwa Nchini kwa kujihusisha na dawa za kulevya 20

3.4 Raia wa Tanzania waliokamatwa nje ya nchi kwa kujihusisha na dawa za kulevya 20

3.5 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya 21

3.6 Uchunguzi wa sampuli zilizodhaniwa kuwa dawa za kulevya 23

3.7 Mashauri ya dawa za kulevya 23

3.8 Uteketezaji wa dawa za kulevya 24

3.9 Utaifishaji wa mali zilizotokana na uhalifu wa dawa za kulevya 24

SURA YA NNE 25

KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION) 25

4.1 Utangulizi 25

4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya 25

4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya 26

4.4 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya 29

4.5 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya 31

SURA YA TANO 38

KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA (HARM REDUCTION) 38

5.1 Utangulizi 38

5.2 Huduma ya matibabu ya Uraibu katika Vitengo vya Afya ya Akili 38

5.3 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa na Unasihi (Medically Assisted Therapy-MAT) 40

5.4 Huduma ya Kupunguza Magonjwa Ambukizi kwa Wajidunga (Needle and Syringe Program-NSP) 43

5.5 Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses) 43
5.6 Huduma za Kisaikolojia 45
5.7 Faida za Matibabu kwa watu wenye Uraibu wa Dawa za Kulevya .. 45
5.8 Asasi za Kiraia zilizowezeshwa na Serikali mwaka 2025 45

SURA YA SITA 46

USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA 46

6.1 Utangulizi 46
6.2 Ushirikiano wa Kitaifa 46
6.3 Ushirikiano wa Kikanda 46
6.4 Ushirikiano wa Kimataifa 47

SURA YA SABA 48

CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE 48

7.1 Utangulizi 48
7.2 Changamoto 48
7.3 Mikakati ya Baadaye 48

VIAMBATA 49

Kiambata Na. I 49
Kiambata Na. II 52

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa Muongo mmoja (mwaka 2016 -2025) 14

Jedwali Namba 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa katika Muongo mmoja Mwaka 2016 hadi 2025 15

Jedwali Na. 3.6: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (Mwaka 2016 hadi 2025).......... 17

Kielelezo Na. 3.7: Kiasi cha heroin na cocaine kilichokamatwa katika Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025 17

Jedwali Na. 3.8: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kwa muongo mmoja (Mwaka 2016 hadi 2025)......... 18

Jedwali Na. 3.10: Dawa nyingine za kulevya zilizokamatwa mwaka 2021 hadi 2025 19

Jedwali Na. 3.11: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2025 21

Jedwali Na. 3.12: Kiasi cha kemikali Bashirifu zilizozuiwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2025.......... 22

Jedwali Na.5.1: Idadi ya Watu wenye Uraibu waliopata Tiba kwenye Vitengo vyaAfya ya Akili Nchini kwa Mwaka 2025 39

Jedwali namba.5.2: Idadi ya watu wenye uraibu waliohudumiwa kwenye vituo vya MAT kuanzia mwaka 2011 hadi 2025 41

Jedwali namba 5.3: Idadi ya watu wenye uraibu waliohudumiwa katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2021 hadi 2025- Tanzania Bara. 43

ORODHA YA VIELELEZO

Kielelezo na. 3.2 kiasi cha bangi na mirungi kilichokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025 14

Kielelezo na. 3.3: Mwenendo wa kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025 15

Kielelezo Na 3.5: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa waliokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025................. 16

Kielelezo Na. 3.7: Kiasi cha heroin na cocaine kilichokamatwa katika Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025 17

Kielelezo Na. 3.9: Mwenendo wa watuhumiwa wa heroin na cocaine waliokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025 18

MAELEZO YA WAZIRI

Mapambano dhidi ya dawa za kulevya yaliendelea kuimarika nchini kwa mwaka 2025. Hii ni kutokana na uwezeshaji mkubwa uliofanywa na Serikali ya awamu ya sita kwa kuimarisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa ya kupambana na dawa za kulevya inayolenga kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa.

Mwaka 2025, jumla ya tani 1,074.72 za dawa za kulevya zilikamatwa katika operesheni zilizofanyika katika maeneo mbalimbali nchini. Dawa hizo zinajumuisha bangi tani 1,014.06, mirungi tani 26.36, skanka tani 3.20, kratom tani 29.52, heroin kilogramu 672.23 cocaine kilogramu 4.89, methamphetamine kilogramu 907.18, MDA gramu 7.82 na MDMA gramu 178.

Bangi iliendelea kukamatwa kwa wingi, hata hivyo, kiasi kilichokamatwa kilipungua kwa asilimia 55.97 ikilinganishwa na mwaka 2024. Hii ni kutokana na uteketezaji wa mashamba ya bangi uliofanyika mwaka 2024, kuimarika kwa udhibiti ikiwemo utoaji elimu kwa jamii inayojihusisha na kilimo cha bangi kuhusu madhara ya kilimo cha zao hilo.

Katika kipindi cha mwaka 2025, kuliibuka aina mpya ya dawa za kulevya aina ya Kratom itokanayo na mmea unaoitwa Mitrogyna speciosa ambapo tani 29.52 zilikamatwa jijini Dar es Salaam. Dawa hii iliingizwa nchini kama mbolea, baada ya uchunguzi ilibainika kuwa ni dawa ya kulevya.

Mirungi ilifuatia katika dawa za kulevya zilizokamatwa, ambapo jumla ya tani 26.36 zilikamatwa. Kiasi hiki kiliongezeka kwa asilimia 42.88 ikilinganishwa na mwaka 2024. Ongezeko hili linaashiria kuimarika kwa operesheni za ufuatiliaji na udhibiti hususan katika maeneo ya mipaka na njia zinazotumika kusafirisha dawa hizo.

Aidha, Serikali iliendelea kuimarisha ukaguzi katika vituo vya forodha, vyombo vya usafiri, kampuni za usafirishaji vifurushi na kwenye kampuni zinazojihusisha na biashara ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa lengo la kudhibiti uchepushwaji. Jumla ya tani 31.76 na lita 183.500 za kemikali bashirifu pamoja na kilogramu 2.36 na Mililita 160 za dawa tiba zenye asili ya kulevya zilikamatwa kufuatia operesheni zilizofanyika.

Kwa upande wa makosa ya dawa za kulevya, jumla ya mashauri 1,124 yalifunguliwa katika Mahakama mbalimbali nchini kwa mwaka 2025. Aidha, pamoja na mashauri yaliyokuwa yakiendelea katika Mahakama mbalimbali nchini, mashauri 1,373 yalitolewa hukumu na Jamhuri ilishinda mashauri 1,058. Kadhalika, mali

zenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 3.3 zilizohusishwa na makosa ya dawa za kulevya zilitaifishwa.

Sambamba na hatua za udhibiti, Serikali iliendelea kutoa huduma za tiba na utengamao kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya. Mwaka 2025, jumla ya watu 85,425 wenye uraibu wa dawa za kulevya walipata tiba kwenye vitengo vya afya ya akili katika hospitali za rufaa za mikoa na Kanda, kliniki za MAT na nyumba za upataji nafuu 'sober house' nchini.

Aidha, juhudi za utoaji wa elimu kwa umma kuhusu tatizo la dawa za kulevya ziliendelea kuimarishwa kupitia kampeni mbalimbali za uelimishaji katika jamii, taasisi za elimu na vyombo vya habari ili kujenga jamii yenye uelewa, maamuzi sahihi na uwezo wa kujilinda dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Inakadiriwa watu milioni 25 walifikiwa na programu mbalimbali za utoaji wa elimu katika mwaka 2025.

Katika kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa, Serikali imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi katika kubadilishana taarifa za kiintelijensia, kujenga uwezo wa kitaasisi pamoja na kuendesha operesheni za pamoja dhidi ya mitandao ya usafirishaji na biashara ya dawa za kulevya.

Pamoja na kuimarika kwa udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya mwaka 2025, Serikali itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ili kuhakikisha Tanzania inakuwa huru bila biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Natoa pongezi kwa wadau walioshiriki kwa namna mbalimbali katika kufanikisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini. Ushirikiano ni silaha kuu ya kushinda vita dhidi ya dawa za kulevya.

Kataa Dawa za Kulevya, Timiza malengo yako!

Prof. Palamagamba J.A Kabudi (Mb)
Waziri wa Nchi,
Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)

DIBAJI

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuimarisha mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya kwa lengo la kulinda afya ya jamii, usalama wa wananchi na maendeleo ya Taifa. Kufuatia dhamira hiyo, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeandaa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya nchini ya mwaka 2025 inayobainisha mwenendo wa tatizo la dawa za kulevya na hatua zinazochukuliwa kukabiliana nalo ili kuwezesha wadau mbalimbali na wananchi kufahamu hali halisi ya tatizo hilo.

Uandaaji wa Taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya ni utekelezaji wa Kifungu cha 60 cha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Na. 5 ya Mwaka 2015, inayoitaka Mamlaka kuandaa na kuwasilisha bungeni taarifa hii kila mwaka.

Taarifa hii ina sura saba zinazoangazia tatizo la dawa za kulevya nchini pamoja na utekelezaji wa mikakati mikuu minne inayoongoza udhibiti na mapambano dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Mikakati hiyo ni kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya, kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya, kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya na kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya.

Aidha, taarifa hii imebainisha mafanikio yaliyopatikana katika operesheni, utoaji wa elimu kwa umma, ushirikishwaji wa jamii sambamba na huduma za matibabu kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya. Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, taarifa hii pia imebainisha maeneo yanayohitaji kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa mapambano dhidi ya dawa za kulevya ni endelevu na yenye matokeo chanya kwa Taifa.

Ni matarajio yangu kuwa, taarifa hii itaendelea kuwa nyenzo muhimu katika kusaidia maamuzi ya kisera, kuimarisha uelewa wa wadau na kuboresha ufanisi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini.

Ninatoa shukrani za dhati kwa taasisi, vyombo vya ulinzi na usalama, wadau wa maendeleo pamoja na wananchi waliochangia kwa namna mbalimbali katika udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya na hivyo kufanikisha maandalizi ya taarifa hii

Aretas J. Lyimo

KAMISHNA JENERALI

MAMLAKA YA KUDHIBITI NA

KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA

Mei, 2026

FAHARASA

ATS	Amphetamine Type Stimulants
DCEA	Drug Control and Enforcement Authority
DEA	Drug Enforcement Adminstration
GCLA	Government Chemist Laboratory Authority
NPS	New Psychoactive Substances
TAA	Tanzania Airports Authority
TAKUKURU	Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa
TCAA	Tanzania Civil Aviation Authority
TFS	Tanzania Forest Services Agency
THC	Tetrahydrocannabinol
TMDA	Tanzania Medicines and Medical Devices Authority
TRA	Tanzania Revenue Authority
UKIMWI	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNODC	United Nations Office on Drugs and Crime
VVU	Virusi vya UKIMWI

SURA YA KWANZA

HALI YA DAWA ZA KULEVYA DUNIANI

1.1 Utangulizi

Sura hii inaeleza kuhusu matumizi na biashara ya dawa za kulevya, dawa mpya za kulevya na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa kutumia dondoo za Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 katika sura ya dunia kwa ujumla.

1.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya Duniani

Taarifa ya hali ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2025, ilionesha kuwa, matumizi ya dawa za kulevya yamefikia viwango vya juu zaidi kuwahi kurekodiwa katika historia. Taarifa hiyo inaonesha kuwa kiwango cha matumizi ya dawa za kulevya kimeendelea kuwa juu zaidi katika eneo la Amerika Kaskazini ukilinganisha na maeneo mengine Duniani. Taarifa hiyo inabainisha kuwa, watu wapatao milioni 316 Duniani, wenye umri wa miaka 15 hadi 64 walitumia angalau aina moja ya dawa za kulevya katika mwaka 2023. Hii ni sawa na takribani asilimia 6 ya watu wote duniani ikiwa ni ongezeko la asilimia 28 la matumizi ya dawa za kulevya ikilinganishwa na miaka kumi (10) iliyopita. Moja ya sababu ya ongezeko hili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya watu duniani.

Mwaka 2023, bangi iliendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumika zaidi duniani, ambapo watu milioni 244 (4.6% ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64) waliripoti kuitumia ndani ya kipindi cha mwaka mmoja uliopita. Miongoni mwa sababu zinazochangia ongezeko hili ni kuhalalishwa kisheria kwa matumizi ya bangi kwa madhumuni yasiyo ya kitabibu katika baadhi ya nchi, zikiwemo Canada, Uruguay, Malta, Luxembourg, Ujerumani na Afrika Kusini. Dawa zilizofuata kwa wingi wa matumizi ni dawa za kulevya jamii ya afyuni zikitumiwa na watu milioni 61 (1.2%), Dawa za kulevya jamii ya amphetamine zikitumiwa na watu milioni 31 (0.6%), Cocaine watu milioni 25 (0.5%) na “ecstasy” milioni 21 (0.4%).

Taarifa hiyo ilionesha kuwa, ongezeko la matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kuleta madhara makubwa kiafya, kijamii na kiuchumi. Katika ripoti hiyo, inakadiriwa kuwa, mwaka 2021, matumizi hayo yalipelekea vifo vya takribani watu milioni 28. Matumizi ya dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga yameendelea kuchochea maambukizi ya VVU na virusi vya homa ya ini aina ya B na C. Kwa mjibu wa taarifa hiyo, watu wapatao milioni 14 duniani walitumia dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga, kati ya watu hao, watu milioni 1.7 waliokutwa na maambukizi ya VVU, watu milioni 6.9 walikuwa na maambukizi ya homa ya ini aina C na watu milioni 1.5 walikuwa na maambukizi ya VVU pamoja na Homa ya in aina C kwa wakati mmoja.

Taarifa hiyo ilieleza pia kuwa, matumizi ya dawa za kulevya huongeza hatari ya kupata magonjwa ya ini, moyo na mishipa ya damu, saratani na magonjwa ya akili. Takribani nusu ya watu wanaotumia dawa za kulevya hukumbwa pia na angalau tatizo moja la afya ya akili. Dawa za kulevya jamii ya afyuni kama vile fentanyl na heroin zimeendelea kusababisha vifo vya watu wengi duniani kutokana na kuzidisha kiasi cha dawa (overdose).

1.3 Matumizi ya Bangi Duniani na Athari zake

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2025, inakadiriwa kuwa watu milioni 244 walitumia bangi mwaka 2023, sawa na asilimia 4.6 ya watu duniani wenye umri wa miaka 15 hadi 64. Katika kipindi cha muongo mmoja uliopita, idadi ya watumiaji imeongezeka kwa asilimia 34, jambo linaloifanya bangi kuendelea kuwa dawa ya kulevya inayotumika zaidi duniani. Taarifa inaonesha kuwa kiwango cha matumizi ya bangi kiko juu zaidi Amerika Kaskazini, ambapo mwaka 2023 takribani asilimia 20.2 ya watu wa umri huo waliripotiwa kuitumia.

Matumizi ya bangi yameendelea kuwa chanzo kikuu cha watu kuingia kwenye huduma za matibabu ya uraibu katika maeneo mbalimbali duniani, ambapo asilimia 42 ya watumiaji wa dawa za kulevya katika mwaka 2021 walikuwa wakitumia bangi. Aidha, mwaka 2023, asilimia 41 ya nchi ziliripoti bangi kuwa dawa kuu inayosababisha watu kuhitaji matibabu. Kwa ngazi ya kikanda, katika Oceania (Australia, Visiwa vya Pasifiki na New Zealand), asilimia 37 ya watu waliokuwa kwenye matibabu waliripoti bangi kuwa tatizo lao kuu, huku Afrika ikiwa na asilimia 32 ya watu waliotaja matumizi ya bangi kama sababu ya kuingia kwenye matibabu.

Ripoti hiyo inaonesha pia kuwa, bidhaa za bangi ikiwemo bangi ya majani, bangi iliyosindikwa (hashish), mafuta ya bangi, bangi za kutengenezwa viwandani na vyakula vyenye viambata vya bangi (Biskuti, keki, pipi) zimeongezeka zaidi jambo linalotishia usalama wa afya Duniani. Katika baadhi ya maeneo, kiwango cha kemikali hatari ya THC katika bangi hizo kimefikia asilimia 70 hadi 80. Taarifa za Bodi ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (INCB) zinaonesha kuwa, bidhaa hizi zenye viwango vikubwa vya THC zinazidi kuenea katika maeneo ya Amerika ya Kusini na nchi za kusini mwa Afrika.

Barani Afrika, matumizi ya bangi yapo juu zaidi katika kanda za Afrika ya Kusini, Magharibi na Kati. Mwaka 2023, kiwango cha matumizi ya bangi ndani ya kipindi cha mwaka mmoja kilikadiriwa kufikia takribani asilimia 10 ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 katika maeneo hayo. Aidha, asilimia 44 ya bangi (bangi kavu na iliyosindikwa) iliyokamatwa duniani mwaka 2023 ilitoka Afrika kiasi ambacho kilizidi kile kilichokamatwa Amerika, Asia na Ulaya. Ripoti inaonesha kuwa, matumizi ya bangi katika umri mdogo huongeza hatari ya kupata matatizo ya akili, ikiwemo msongo wa mawazo (stress), sonona (depression), wasiwasi (Anxiety),

kuchanganyikiwa (Psychosis), Matatizo ya kumbukumbu na ufahamu na ukosefu wa umakini.

1.3.1 Uhalalishaji wa Bangi na Athari Zake

Hadi kufikia Desemba 2024, nchi za Canada, Uruguay, na majimbo 28 ya Marekani tayari yalikuwa yamehalalisha kilimo, uuzaji, na matumizi ya bangi kwa madhumuni yasiyo ya kitabibu. Katika sehemu nyingi za Canada na Marekani, uhalalishaji huo ulifanyika kwa lengo la kujipatia faida kupitia biashara hiyo, wakati nchini Uruguay serikali imeendelea kudhibiti kwa kuuza kwa kiasi kidogo kwa watu wazima tu. Barani Ulaya, nchi kama Malta (iliyohalalisha mwaka 2021), Luxembourg (mwaka 2023), na Ujerumani (mwaka 2024) zinaruhusu watu wazima kulima miche michache nyumbani na kumiliki kiasi kidogo cha bangi kwa matumizi binafsi. Nchini Afrika Kusini, watu wazima wanaruhusiwa kulima, kumiliki, na kutumia bangi majumbani mwao, na pia kubeba kiasi kidogo hadi maeneo ya umma. Nchi kama Uholanzi na Uswisi bado zinaendelea kufanya utafiti juu ya athari za uhalalishaji wa bangi.

Ushahidi kutoka nchi zilizohalalisha matumizi yasiyo ya kitabibu ya bangi unaonesha ongezeko la idadi ya watumiaji, jambo linalochangia hatari kubwa za kiafya, hasa miongoni mwa vijana. Bidhaa zenye kiwango kikubwa cha THC, zimeonekana kuongeza hatari ya utegemezi, kusababisha matatizo ya akili, na kuhitaji kulazwa hospitalini. Hali hii imechangia ongezeko la watu wenye matatizo ya akili yanayohusiana na bangi, ikiwemo wasiwasi, huzuni, kuchanganyikiwa (psychosis), na mawazo ya kujiua. Matokeo haya yanaonyesha wazi kuwa uhalalishaji wa bangi haupunguzi hatari za kiafya, bali unaweza kuongeza uwezekano wa watu wengi zaidi kuingia kwenye matumizi hatarishi, hususan miongoni mwa makundi yaliyo hatarini.

Taarifa ya INCB inabainisha kuwa kuruhusu matumizi ya bangi kwa madhumuni yasiyo ya kitabibu ni kinyume cha sheria za kimataifa za kudhibiti dawa za kulevya, hasa Mkataba wa Kimataifa wa Dawa za Kulevya wa mwaka 1961 (Single Convention on Narcotic Drugs of 1961). Ripoti hiyo inafuatilia nchi ambazo tayari zimehalalisha au zinafikiria kuhalalisha bangi, na inaonya kuhusu athari mbaya zinazosababishwa na sera ya uhalalishaji wa bangi.

1.4 Heroin

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia mwaka 2025, takribani watu milioni 61 duniani (asilimia 1.2 ya idadi ya watu) walitumia dawa za kulevya jamii ya afyuni (opioids) mwaka 2023. Kati ya hao, takribani watu milioni 30 walitumia heroin. Kwa ujumla, watumiaji wa afyuni walifikia asilimia 0.57 ya watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 duniani. Taarifa kutoka nchi 135 zinaonesha kuwa mwaka

2023, mraibu mmoja kati ya watatu waliokuwa wanatibiwa alikuwa anatumia afyuni. Dawa hizi zinaendelea kusababisha madhara makubwa, zikichangia takribani theluthi mbili ya vifo vyote vinavyohusiana moja kwa moja na dawa za kulevya duniani, hasa kutokana na kuzidisha kiasi cha dawa (overdose).

Ripoti inaonesha uzalishaji wa mimea inayotumika kutengenezea dawa aina ya afyuni duniani ulipungua kwa asilimia 74. Upungufu huu ulitokana na kupigwa marufuku kwa uzalishaji wa mimea hiyo nchini Afghanistan mwezi Aprili 2022, kulikopelekea upungufu wa mimea hiyo kwa takribani asilimia 95. Hali hii aliathiri kwa kiwango kikubwa uzalishaji wa dawa za kulevya aina ya heroin duniani. Mwaka 2024, Myanmar ilikuwa mzalishaji mkuu wa heroin duniani, ikichangia karibu nusu ya uzalishaji. Hata hivyo, mwaka 2023, njia ya Balkan iliendelea kuwa njia kuu ya usafirishaji wa heroin kwenda masoko ya Ulaya. Licha ya mabadiliko katika uzalishaji, matumizi ya heroin yanaendelea kuwa changamoto kubwa ya kiafya kwa umma. Nchini Marekani, matumizi ya Fentanyl yanaendelea kuwa tatizo kubwa, huku vifo vinavyotokana na kuzidisha kiasi cha dawa hiyo (over dose) vikiripotiwa kwa kiwango cha juu.

Katika maeneo mengine ikiwemo Afrika Kaskazini, Magharibi, Mashariki ya Kati na Asia ya Kusini-Magharibi matumizi yasiyo ya kitabibu ya Tramadol yaliongezeka na kuibua changamoto mpya za kiafya na kijamii. Aidha, kuna ongezeko la matumizi ya Nitazene, ambayo ni afyuni ya viwandani yenye nguvu zaidi ya Fentanyl na hutumika kama mbadala wa heroin. Mwishoni mwa mwaka 2023, Nitazene ilisababisha mamia ya vifo, barani Ulaya na Amerika Kaskazini. Taarifa zinaonesha pia uwepo wake katika eneo la Oceania (Australia, Visiwa vya Pasifiki na New Zealand) na Afrika, ambako wakati mwingine huchanganywa na dawa nyingine na kutumika kwa kuvuta (kush).

1.5 Hali ya Biashara na Matumizi ya Cocaine Duniani

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025, inaonesha kuwa biashara ya cocaine duniani limefikia viwango ambavyo havijawahi kushuhudiwa. Inakadiriwa kuwa watu milioni 25 walitumia cocaine mwaka 2023, ikilinganishwa na milioni 17 muongo mmoja uliopita. Kiwango cha matumizi ya cocaine kwa watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64 kilifikia takribani asilimia 0.47 ya idadi ya watu duniani. Hali hii inaonesha kuendelea kuongezeka kwa matumizi licha ya kuimarishwa kwa juhudi za udhibiti wa biashara hiyo.

Uzalishaji wa cocaine duniani ulifikia tani 3,708 mwaka 2023, ambayo ni zaidi ya theluthi moja ya uzalishaji wa mwaka uliopita ikiwa ni kiwango cha juu zaidi kuwahi kurekodiwa. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa kilimo cha mmea wa coca unaotumika kutengenezea Cocaine pamoja na uzalishaji wa cocaine hususani nchini Colombia. Hata hivyo, upatikanaji mkubwa wa dawa hiyo unaashiria kuwa uzalishaji bado umeongezeka licha ya udhibiti.

Amerika Kaskazini pamoja na Ulaya Magharibi na Kati zimeendelea kuwa masoko makuu ya cocaine. Aidha, matumizi na njia za usafirishaji zimeendelea kupanuka kuelekea Afrika na baadhi ya maeneo ya Asia. Afrika Magharibi imeibuka kama kitovu cha kupitisha cocaine kutoka Amerika Kusini kuelekea Ulaya, huku zaidi ya asilimia 80 ya shehena kubwa zinazokamatwa zikihusishwa na usafirishaji wa njia ya bahari katika eneo hilo. Athari za kupitisha dawa hizi pia zimechangia kuongezeka kwa matumizi ya ndani katika baadhi ya nchi za Afrika, wakati Ulaya Magharibi na Kati zikishuhudia kuongezeka kwa mahitaji ya matibabu na vifo vinavyohusishwa na cocaine.

1.6 Dawa Tiba zenye Asili ya Kulevya

Dawa hizi hutengenezwa na kusambazwa kisheria kwa ajili ya matibabu chini ya usimamizi wa kitaalamu. Hata hivyo, zinakuwa tishio la kiafya zinapotumiwa bila ushauri wa daktari, au kwa madhumuni yasiyo ya kitabibu. Matumizi mabaya ya dawa tiba jamii ya afyuni, benzodiazepine na dawa nyingine zinazodhibitiwa yanaweza kusababisha uraibu, vifo kutokana na kuzidisha kiasi cha matumizi "*overdose*" na madhara ya muda mrefu kiafya. Matumizi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya ni suala linalokua kwa kasi na kuongeza ukubwa wa dawa za kulevya duniani.

Matumizi yasiyo ya kitabibu ya Tramadol yameongezeka hususani Afrika Magharibi na Kati, kupitia mifumo isiyo rasmi ya usambazaji. Aidha, dawa aina ya codeine na diazepam zimekuwa zikichepushwa na kusambazwa katika maeneo mbalimbali. Ketamine nayo imepata soko la matumizi yasiyo ya kitabibu katika baadhi ya nchi za Asia na Ulaya, huku matumizi ya muda mrefu yakihusishwa na madhara makubwa ya njia ya haja ndogo na matatizo ya kisaikolojia.

Mtu mmoja (01) kati ya 12 wenye tatizo la uraibu wa dawa tiba hupata matibabu duniani, na hali ni mbaya zaidi kwa wanawake. Ripoti ya INCB ya mwaka 2024 inaonesha kuwa uchepushaji katika usambazaji wa dawa tiba, udhaifu wa mifumo ya ufuatiliaji ya dawa na uwepo wa maduka ya dawa mtandaoni yasiyo halali ni changamoto kuu, huku ikisisitiza umuhimu wa kuhakikisha upatikanaji wa dawa kwa matumizi halali ya kitabibu pamoja na kuzuia uchepushaji.

1.7 Dawa Mpya za Kulevya (New Psychoactive Substances - NPS)

Dawa mpya za kulevya ni dawa zinazotengenezwa kwa kuiga kemikali zilizopo kwenye dawa za kulevya zinazodhibitiwa kimataifa kwa lengo la kuficha uhalisia wa dawa hizo ili kukwepa mkono wa sheria. Dawa hizi hufanyiwa mabadiliko ya kimuundo wa kikemikali mara kwa mara ili kukwepa udhibiti, jambo linalozifanya kuwa na athari zisizotabirika na mara nyingi hatarishi kwa afya ya mtumiaji. Dawa hizi zimeendelea kuenea kwa kasi katika masoko ya dawa za kutengenezwa kwenye maabara duniani.

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025, ilionesha kuwa dawa mpya aina 527 ziligunduliwa duniani hadi kufikia mwaka 2023, zikiwemo aina 56 zilizogunduliwa katika mwaka 2023 pekee. Ingawa kasi ya kuibuka kwa dawa mpya imepungua ukilinganisha na miaka ya awali, kuendelea kuonekana kwa aina mpya kunaonesha uwezo mkubwa wa soko hili kubadilika. Dawa hizi zinazotengenezwa maabara hujumuisha bangi, vichangamshi na dawa jamii ya afyuni ikiwemo Nitazene zimebainishwa kuwa hatari zaidi kutokana na sumu kali na uwezekano mkubwa wa kusababisha vifo kwa "overdose".

Tofauti na dawa za asili zinazotegemea kilimo, dawa mpya za kulevya huleta changamoto katika udhibiti kutokana na kuzalishwa kwa kiasi kidogo na kuuzwa kwa njia ya mitandao ya siri "dark web" na kampuni za usafirishaji vifurushi. INCB katika ripoti yake ya mwaka 2024 inaonesha kuwa ugunduzi wa kemikali mpya ambazo hazijaorodheshwa rasmi ni changamoto kubwa ya kisheria na kiudhibiti. Hivyo, bodi hiyo inasisitiza umuhimu wa kuimarisha ufuatiliaji wa kemikali bashirifu pamoja na kuboresha ushirikiano wa kimataifa.

Mahitaji ya dawa hizi mara nyingi huchochewa na dhana potofu kwamba ni halali kisheria, bei nafuu au hazigunduliki katika vipimo vya dawa na hutumika zaidi miongoni mwa vijana na katika mazingira ya burudani za usiku. Hata hivyo, kiwango halisi cha matumizi ni vigumu kupima kwa sababu aina za dawa hubadilika haraka. Madhara yake ni makubwa na yasiyotabirika, yakihusisha sumu kali, matatizo ya akili na vifo vinavyotokana na "overdose", huku mifumo ya matibabu ikiendelea kuwa na uwezo mdogo wa kugundua na kuhudumia watu wenye uraibu.

1.8 Dawa za Kulevya Jamii ya Amphetamine (Amphetanine Type Stimulants-ATS)

Kundi hili linajumuisha dawa kama Amphetanine, Methamphetamine na Ecstasy ambazo ni vichangamshi vinavyoathiri mfumo wa fahamu wa mtumiaji kwa kubadili jinsi ya kufikiri, kuhisi na kutenda. Taarifa ya Dawa za Kulevya Duniani ya mwaka 2025, inaonesha takribani watu milioni 30 walitumia ATS mwaka 2023. Ukamataji wa dawa hizi ulifikia kiwango cha juu zaidi kuwahi kurekodiwa, ukichangia karibu nusu ya ukamataji wote wa dawa za kutengenezwa kwenye maabara duniani, jambo linaloashiria uzalishaji mkubwa na mahitaji yanayoendelea kuongezeka.

Biashara ya Methamphetamine inaongoza katika ATS, ikizalishwa kwa kiwango kikubwa katika Asia Mashariki na Amerika Kaskazini, hasa nchini Mexico. Amphetamine bado inatumika kwa wingi katika baadhi ya maeneo ya Ulaya na Mashariki ya Kati. Matumizi ya muda mrefu ya methamphetamine yanahusishwa na matatizo ya akili, kukosa utulivu na magonjwa ya moyo. Mahitaji ya huduma za matibabu kwa waraibu wa vichangamshi yameongezeka katika maeneo mbalimbali, lakini tiba za dawa bado ni chache na huduma hutegemea zaidi tiba za kisaikolojia.

Methamphetamine

1.9 Jinsia na Matumizi ya Dawa za Kulevya

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 inaangazia tofauti za matumizi ya dawa za kulevya na athari zake kulingana na jinsia.Taarifa hiyo inaonesha kuwa wanaume wanaotumia dawa za kulevya ni wengi kuliko wanawake, ambapo takribani robo tatu ya watumiaji wa bangi, cocaine na heroin ni wanaume. Hata hivyo, wanawake wako katika hatari ya kupata madhara makubwa zaidi wanapoanza kutumia dawa hizo, hali inayochangiwa na sababu za kibaiolojia. Kwa ujumla, wanawake huanza matumizi katika umri mkubwa zaidi kuliko wanaume, lakini baada ya kuanza huongeza matumizi ya aina mbalimbali za dawa kwa kasi zaidi na huwa katika hatari ya kupata utegemezi au uraibu wa dawa hizo kwa haraka zaidi kuliko wanaume. Katika eneo la Amerika Kaskazini, pengo la matumizi ya bangi kati ya wanaume na wanawake linaendelea kupungua, ambapo katika maeneo yenye viwango vya juu vya matumizi, jinsia zote mbili sasa zinatumia bangi kwa idadi inayokaribiana.

Mwaka 2023, upatikanaji wa huduma za matibabu kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya uliendelea kuwa mdogo zaidi kwa wanawake kuliko kwa wanaume. Takwimu zinaonesha kuwa ni mwanamke mmoja (01) tu kati ya 18 aliyepata

matibabu, ikilinganishwa na mwanaume mmoja (01) kati ya saba (07). Wanawake wanakabiliwa na unyanyapaa mkubwa zaidi, fedheha, na ubaguzi unaohusiana na matumizi ya dawa za kulevya, jambo ambalo mara nyingi huwakatisha tamaa kutafuta msaada. Aidha, wanakabiliwa na vikwazo vingi katika kupata huduma za matibabu na huduma nyingine za afya, hususan zinazoshughulikia mahitaji yao maalum. Wanawake wanaojidunga dawa za kulevya wako katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa VVU na homa ya ini aina ya B na C ikilinganishwa na wanaume.

Ripoti hiyo inaonesha kuwepo kwa uhusiano wa karibu kati ya matumizi ya dawa za kulevya na vitendo vya ukatili, hususan ukatili wa kijinsia. Inaelezwa kuwa watu wanaotumia dawa za kulevya, hasa wale waliopo katika makundi yaliyo hatarini au yaliyotengwa kijamii, hukumbana na aina mbalimbali za ukatili unaoweza kutokea kutoka kwa wenza wa karibu, marafiki, au watu wanaohusika katika biashara ya dawa hizo.

Aidha, wanawake wanaotumia dawa za kulevya pamoja na wale walio katika mahusiano na wanaume wanaotumia dawa hizo wako katika hatari kubwa zaidi ya kufanyiwa ukatili na wenza wao. Katika baadhi ya matukio, wanawake hujikuta wakianza au kuendelea kutumia dawa za kulevya kama njia ya kukabiliana na msongo wa mawazo, manyanyaso na vitendo vya ukatili wanavyovipata katika mahusiano yao. Hali hii inaweza kuchochea na kuongeza tatizo la utegemezi wa dawa za kulevya na hivyo kuongeza zaidi athari za kiafya, kisaikolojia na kijamii.

1.10 Dawa za Kulevya na Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia

Ukuaji wa Sayansi na teknolojia umewezesha uzalishaji wa dawa za kulevya kwa mwaka mzima bila kutegemea misimu ya kilimo. Hii inatokana na uzalishaji wa dawa za kulevya za viwandani (synthetic drugs) katika maabara bubu. Aidha, maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano, hususan mitandao ya kijamii na intaneti, yamerahisisha usambazaji na upatikanaji wa dawa za kulevya. Watu wanaweza kuwasiliana na wauzaji kwa siri "*dark webs*", kuagiza dawa mtandaoni na kuzipata bila kutambulika kwa urahisi. Majukwaa haya hutumia mifumo ya mawasiliano ya kificho na malipo kupitia sarafu za kidijitali (crypto currencies) ili kupunguza ufuatiliaji wa kifedha.

Biashara ya dawa za kulevya mtandaoni pia hufanyika kwa kupitia usafirishaji wa vifurushi vidogo katika huduma za posta na usafirishaji wa mizigo midogo, hali inayopunguza hatari ya kukamatwa kwa shehena kubwa. Aidha, maendeleo ya sayansi na teknolojia yamechangia katika kufanya mabadiliko ya miundo ya kemikali na kutengeneza dawa mpya za kulevya zinazoendelea kuongeza ugumu wa kudhibiti. Hata hivyo, sayansi na teknolojia hutumika katika kupambana na mwenendo huu. Uchunguzi wa maabara husaidia kutambua dawa mpya

zinazoibuka, uchunguzi wa kimtandao hufuatilia mitandao ya usambazaji, na uchambuzi wa takwimu husaidia kufuatilia mienendo ya matumizi na fedha.

1.11 Matumizi ya Dawa za Kulevya miongoni mwa Wanafunzi

Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 inaonesha kuwa matumizi ya dawa za kulevya katika umri mdogo yana madhara makubwa, yanayopelekea vifo pamoja na changamoto za kiafya na kijamii. Vijana hutumia dawa za kulevya kwa kiwango kinachofanana au kuzidi watu wazima, hususani wanafunzi wa shule za sekondari wenye umri wa miaka 15 na 16 kuliko ilivyo kwa idadi ya watu wazima.

Nchini Guinea, asilimia 0.94 ya wanafunzi waliohojiwa waliripoti kutumia "kush" na kuifanya kuwa dawa ya tatu kwa matumizi baada ya bangi na viyeyushi (inhalants). Katika eneo la Oceania (Australia, Visiwa vya Pasifiki na New Zealand), matumizi ya bangi miongoni mwa wanafunzi wa miaka 15 na 16 ni asilimia 13, kiwango ambacho ni cha juu zaidi ukilinganisha na wastani wa dunia wa asilimia 4.4. Barani Ulaya, matumizi ya bangi miongoni mwa vijana wa miaka 15 na 16 bado yako juu zaidi kuliko watu wenye umri wa miaka 15 hadi 64.

Tafiti zinaonesha kuwa, matumizi ya bangi katika kipindi cha ujana yanaweza kuathiri uwezo wa kufikiri, kuvuruga maendeleo ya kitaaluma na binafsi, na kupunguza ufanisi katika masomo pamoja na fursa za ajira baadaye maishani. Matumizi ya mara kwa mara, hasa yanapoanza katika umri mdogo, yanaweza pia kuongeza hatari ya kuchanganyikiwa, matatizo ya hisia na wasiwasi, hali inayoathiri ukuaji na maendeleo. Taarifa ya Dawa za Kulevya ya Dunia ya mwaka 2025 inaeleza kuwa sababu zinazochochea matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana ni malezi duni, kutelekezwa utotoni, urahisi wa upatikanaji wa dawa na sababu binafsi. Hivyo, juhudi za kinga huwa na ufanisi zaidi zinapolenga kushughulikia sababu za mtu binafsi pamoja na mazingira kwa mapana, hususan katika familia na shule.

SURA YA PILI

MIKAKATI YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA NCHINI

2.1 Utangulizi

Udhibiti wa tatizo la dawa za kulevya hufuata Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya namba 5 ya mwaka 2015 na miongozo ya Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC). Kuna mikakati mikuu minne inayoongoza jitihada za mapambano dhidi ya dawa za kulevya nchini, ambayo ni; Kupunguza upatikanaji wa dawa za kulevya (supply reduction), Kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya (demand reduction), Kupunguza madhara ya matumizi ya dawa za kulevya (harm reduction) na Kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa (National, Regional and International Cooperation). Sura hii inaelezea mikakati hiyo ambayo utekelezaji wake umeainishwa katika sura zinazofuata.

2.2 Kudhibiti Upatikanaji wa Dawa za Kulevya (Supply Reduction)

Lengo la mkakati huu ni kudhibiti uingizaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya nchini. Upatikanaji wa dawa za kulevya unahusisha kilimo, utengenezaji, uingizaji na usambazaji kupitia mipaka ya nchi kavu, majini na anga. Utekelezaji wa mkakati huu unahusisha; Ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa kuhusu biashara ya dawa za kulevya, ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya, usimamiaji wa sheria ya dawa za kulevya nchini, udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya pamoja na kuratibu uteketezaji wa dawa za kulevya.

2.3 Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya (Demand Reduction)

Mkakati huu umejikita katika utoaji wa elimu ili kuifanya jamii kujitambua na kujiepusha na matumizi na biashara ya dawa za kulevya nchini. Katika utekelezaji wa mkakati huu Mamlaka inaratibu uelimishaji juu ya tatizo la dawa za kulevya katika jamii, ikiwa ni pamoja na kuandaa miongozo ya uelimishaji, kuwaandaa na kuwawezesha watoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya, kuratibu asasi zinazotoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa jamii, kuratibu uanzishwaji na uendeshaji wa klabu za dawa za kulevya na kuhuisha maudhui ya dawa za kulevya kwenye mitaala ya elimu.

2.4 Kupunguza Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya (Harm Reduction)

Lengo la mkakati huu ni kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya. Katika mkakati huu Mamlaka inaratibu huduma za matibabu kwa waraibu wa dawa za kulevya, inaratibu huduma maalumu za kugawa mabomba kwa waraibu wanaojidunga kuzuia maambukizi ya magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya damu (Needle and Syringe Program-NSP), maandalizi ya miongozo ya matibabu, usimamizi shirikishi katika vituo vinavyotoa huduma za tiba na unasihi pamoja na na utoaji elimu ya kupunguza madhara kwa waraibu wa dawa za kulevya

2.5 Kuimarisha Ushirikiano wa Kitaifa, Kikanda na Kimataifa (National, Regional and International Cooperation)

Tatizo la dawa za kulevya ni suala mtambuka linalohusisha mitandao ya kihalifu iliyopo nchi mbalimbali duniani, hivyo mapambano dhidi ya tatizo hili yanahitaji ushirikiano na nguvu za pamoja kuanzia ngazi ya kitaifa, kikanda na kimataifa.

Katika utekelezaji wa mkakati huu masuala yafuatayo huzingatiwa; Utekelezaji wa mikataba na miongozo ya kitaifa, kikanda na kimataifa katika udhibiti wa dawa za kulevya; Ubadilishanaji wa taarifa za kiintelejensia na uzoefu baina ya mataifa kuhusu udhibiti wa dawa za kulevya na kushiriki mafunzo ya pamoja.

Kamishna Jenerali akiwa na wadau wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya

SURA YA TATU

UDHIBITI WA UPATIKANAJI WA DAWA ZA KULEVYA (SUPPLY REDUCTION)

3.1 Utangulizi

Sura hii imejikita katika kuelezea jitihada zilizofanyika katika kudhibiti uzalishaji, usambazaji, uingizaji, matumizi na upatikanaji wa dawa za kulevya nchini. Mamlaka kwa kushirikiana na vyombo vingine vya ulinzi na usalama, wadau na wananchi imefanya operesheni mbalimbali, upelelezi, ufuatiliaji na uendeshaji wa mashauri ya dawa za kulevya pamoja na uteketezaji wa dawa hizo. Aidha, imefanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ili kudhibiti uchepushaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya.

3.2 Operesheni za Ukamataji wa Dawa za Kulevya kwa Mwaka 2025

Operesheni mbalimbali zilizofanyika zilifanikisha kukamata dawa za kulevya za mashambani ambazo ni bangi na mirungi pamoja na dawa za viwandani ambazo ni heroin, cocaine, methamphetamine, MDA, MDMA, kemikali bashirifu, dawa tiba zenye asili ya kulevya na dawa mpya ya kulevya aina ya Kratom. Mafanikio ya ukamataji huo yameainishwa kama ifuatavyo: -

3.2.1 Bangi

Mwaka 2025 kiasi cha tani 1,014.06 za bangi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 7,715, kati ya hao wanaume 7,014 na wanawake 701. ***(Jedwali Na. 3.1 na 3.4 pamoja na Kielelezo Namba 3.2 na 3.3 na 3.5).***

3.2.1.1 Bangi aina ya *'skanka'*

"Skanka" ni bangi chotara ambayo imetokana na bangi aina ya "*Cannabis sativa*" na "*Cannabis indica*" yenye kiasi kikubwa cha kemikali aina ya (Tetrahydrocannabinol -THC) inayoingizwa nchini ikitokea nchi za kusini mwa Afrika. Aina hii ya bangi huchanganywa kwenye sigara na kwenye vyakula '*edibles*' kama biskuti '*cookies*' na keki vinavyotengenezwa na wahalifu nyumbani na viwanda bubu kwa lengo la kukwepa mkono wa Sheria. Mwaka 2025, tani 3.20 zilikamatwa zikiwemo kilogramu 9.82 zilizochanganywa kwenye biskuti na keki, zikihusisha watuhumiwa 137 kati ya hao wanaume 116 na wanawake 21.

Tani 2.7 za bangi aina ya 'skanka' zilizokamatwa

3.2.2 Mirungi

Kiasi cha tani 26.36 za mirungi zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 1,458 kati ya hao wanaume 1,265 na wanawake 193. (***Rejea Jedwali Na.3.1 na 3.4 pamoja na Kielelezo Namba 3.2 na 3.3 na 3.5)***

Jedwali Na. 3.1: Kiasi cha Bangi na Mirungi Kilichokamatwa Nchini kwa Muongo mmoja (mwaka 2016 -2025)

Mwaka	Bangi (Tani)	Mirungi (Tani)
2016	68.23	21.64
2017	52.19	67.81
2018	24.30	8.96
2019	21.51	9.07
2020	13.23	11.80
2021	22.74	10.93
2022	20.58	15.23
2023	1,757.56	202.74
2024	2,303.20	18.45
2025	1,014.06	26.36

Chanzo: Kanzi data DCEA 2025

Kielelezo na. 3.2 Kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025



	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024	2025
Bangi	68.23	52.19	24.3	21.51	13.23	22.74	20.58	1,757.56	2,303.20	1,014.06
Mirungi	21.64	67.81	8.96	9.07	11.8	10.93	15.23	202.74	18.45	26.36

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Kielelezo na. 3.3: Mwenendo wa kiasi cha Bangi na Mirungi kilichokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025



	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023	2024	2025
Bangi	68.23	52.19	24.3	21.51	13.23	22.74	20.58	1,757.56	2,303.20	1,014.06
Mirungi	21.64	67.81	8.96	9.07	11.8	10.93	15.23	202.74	18.45	26.36

Chanzo:Kanzi Data DCEA 2025

Takwimu katika Kielelezo namba 3.2 na 3.3 vinaonesha kiasi cha bangi kilichokamatwa mwaka 2025 kimepungua ukilinganisha na mwaka 2024. Hii ni kutokana na uteketezaji wa mashamba makubwa ya bangi uliofanyika mwaka 2024, kuimarika kwa jitihada za udhibiti ikiwemo utoaji elimu kwa jamii. Aidha, kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2025 kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024 kutokana na ushirikiano kutoka kwa wanajamii kwa kutoa taarifa zilizofanikisha ukamataji wa mirungi hususan inayotoka nchi jirani.

Jedwali Namba 3.4: Idadi ya Watuhumiwa wa Bangi na Mirungi Waliokamatwa katika Muongo mmoja Mwaka 2016 hadi 2025

Mwaka	Watuhumiwa – Bangi	Watuhumiwa – Mirungi
2016	17,889	2,397
2017	11,528	1,797
2018	9,744	1,185
2019	8,865	1,170
2020	7,601	1,156
2021	9,484	1,395
2022	10,277	1,491
2023	8,803	1,179

Mwaka	Watuhumiwa – Bangi	Watuhumiwa – Mirungi
2024	7,981	1,256
2025	7,715	1,458

Chanzo:Kanzi Data DCEA 2025

Kielelezo Namba 3.5: Mwenendo wa Idadi ya Watuhumiwa waliokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025



Chanzo:Kanzi Data DCEA 2025

Kielelezo Namba 3.5 kinaonesha idadi ya watuhumiwa wa bangi waliokamatwa 2025 imepungua ikilinganishwa na mwaka 2024. Hii ni kutokana na kuimarika kwa jitihada za utoaji elimu kwa jamii kuhusu tatizo la dawa za kulevya. Aidha, idadi ya watuhumiwa wa mirungi waliokamatwa 2025 iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024 baada ya kubaini mbinu mpya za usafirishaji uliofanikisha ukamataji huo.

3.2.3 Heroin

Jumla ya kilogramu 672.23 za heroin zilikamatwa nchini mwaka 2025 zikiwahusisha watuhumiwa 63, kati ya hao wanaume 54 na wanawake tisa (09). (Rejea Jedwali Namba 3.6, na 3.8 pamoja na Kielelezo Namba 3.7 na 3.9)

3.2.4 Cocaine

Kiasi cha kilogramu 4.89 za Cocaine zilikamatwa mwaka 2025 zikiwahusisha watuhumiwa 10 kati ya hao wanaume tisa (09) na mwanamke mmoja (01). (Rejea Jedwali 3.6 na 3.8).Kielelezo3.7 na 3.9

Jedwali Na. 3.6: Kiasi cha Heroin na Cocaine Kilichokamatwa Nchini kwa muongo mmoja (Mwaka 2016 hadi 2025)

Mwaka	Kiasi cha Heroin (Kg)	Kiasi cha Cocaine (Kg)
2016	42.26	18.52
2017	185.56	4.14
2018	16.94	7.67
2019	55.35	10.34
2020	349.81	4.52
2021	1,124.52	0.81
2022	254.71	1.73
2023	1,314.28	3.04
2024	433.16	0.85
2025	672.23	4.89

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Kielelezo Na. 3.7: Kiasi cha heroin na cocaine kilichokamatwa katika Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025



Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Takwimu katika kielelezo namba 3.7 zinaonesha kuwa kiasi cha heroin na cocaine kilichokamatwa mwaka 2025 kimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024. Hali hii imetokana na kuimarika kwa jitihada za ukamataji na elimu kwa jamii iliyohamasisha wananchi kutoa taarifa za wanaojihusisha na biashara ya dawa za kulevya.

Jedwali Na. 3.8: Idadi ya Watuhumiwa wa Heroin na Cocaine waliokamatwa kwa muongo mmoja (Mwaka 2016 hadi 2025)

Mwaka	Heroin	Cocaine
2016	716	263
2017	1,005	243
2018	463	148
2019	318	31
2020	428	80
2021	588	100
2022	409	122
2023	196	32
2024	172	41
2025	63	10

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Kielelezo Na. 3.9: **Mwenendo wa watuhumiwa wa heroin na cocaine waliokamatwa kwa kipindi cha Muongo mmoja mwaka 2016 hadi 2025**



Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa na heroin na cocaine kwa mwaka 2025 imepungua kutokana na kushuka kwa biashara na matumizi ya dawa hizo pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa tatizo la dawa za kulevya kwa wananchi.

3.2.5 Methamphetamine 'Meth'

Methamphetamine inayojulikana kwa jina la mtaani kama 'Chumvi' ilianza kuingizwa nchini miaka ya karibuni. Dawa hii imeendelea kukamatwa ambapo mwaka 2025 zilikamatwa kilogramu 907.18 ikihusisha watuhumiwa watatu (03) wote wakiwa wanaume.

3.2.6 Dawa Nyingine za Kulevya

Miaka ya hivi karibuni kumeibuka uingizaji wa dawa ngeni za kulevya hapa nchini ambazo ni pamoja na Methylenedioxyamphetamine (MDA) na Methylenedioxymethamphetamine (MDMA). Dawa hizi hutengenezwa kwa kutumia kemikali bashirifu pekee ambapo Mwaka 2025, kiasi cha gramu 7.82 za MDA na gramu 178 za MDMA zilikamatwa.

Jedwali Na. 3.10: Dawa nyingine za kulevya zilizokamatwa mwaka 2021 hadi 2025

Na.	Mwaka	Methamphetamine (Kg)	Skanka (Kg)	Cannabisresin (Kg)	MDPV (Kg)	Mescaline (Gramu)	MDA (Gm)	MDMA (Gm)
1	2021	430.77	-	-	-	-	-	-
2	2022	0.97	-	-	-	56	-	-
3	2023	2,410.82	426.60	-	-	-	-	-
4	2024	1,729.20	4,168.89	1.00	5	560.8	-	-
5	2025	907.179	3,196.12	-	-	-	7.82	178

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

3.2.7 Dawa Mpya ya Kulevya Kratom (Mitragyna speciosa)

Hii ni dawa mpya ya kulevya inayotokana na mmea wa *Mitragyna speciosa*. Tani 29.52 za Kratom zilikamatwa kwa mara ya kwanza mwaka 2025 zikiingizwa nchini kama mbolea. Dawa hizi zilikamatwa zikiwa kwenye makontena mawili katika bandari ya Dar es Salaam yakihusisha watuhumiwa saba (7), kati ya hao sita (6) wanaume na mwanamke mmoja (1).

Tani 29.52 za Kratom zilizokamatwa jijini Dar es Salaam

3.3 Raia wa Kigeni waliokamatwa Nchini kwa kujihusisha na dawa za kulevya

Mwaka 2025, raia wa kigeni 14 walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na dawa za kulevya kutoka nchi za China 02, Lebanon 01, Congo 01, Sri Lanka 02, Uingereza 02, Marekani 01, Nigeria 01, Ujerumani 01, Kenya 01, Msumbiji 01 na Uganda 01.

3.4 Raia wa Tanzania waliokamatwa nje ya nchi kwa kujihusisha na dawa za kulevya

Watanzania wameendelea kukamatwa wakijihusisha na biashara ya dawa za kulevya wakiwa nje ya nchi. Takwimu za mwaka 2025 zinaonesha jumla ya

watanzania 28 walikamatwa kama ifuatavyo: Botswana wawili (02), Mauritius mmoja (01) Japan mmoja (01), Zambia 20, Msumbiji wawili (02), Ufaransa mmoja (01) na Shelisheli mmoja (01).

3.5 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba Zenye Asili ya Kulevya

3.5.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu (Precursor Chemicals)

Kemikali bashirifu ni kemikali halali zinazotumika katika sekta mbalimbali za uzalishaji ikiwemo kutengeneza dawa tiba, mafunzo kwa vitendo katika taasisi za elimu, kilimo, kuchenjua madini na shughuli nyinginezo. Kemikali hizi huweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya iwapo zitachepushwa na hivyo hufanyiwa ufuatiliaji na ukaguzi ili kudhibiti uchepushwaji wake.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ya mwaka 2025, kampuni za kemikali 127 ziliingiza jumla ya tani 14,747.25 na lita 7,943,019.56 za Kemikali bashirifu kwa kuzingatia Sheria na taratibu za uingizaji wa kemikali nchini.

Jedwali Na. 3.11: Mwenendo wa Uingizaji wa Kemikali Bashirifu Nchini kuanzia mwaka 2017 hadi 2025

Mwaka	Idadi ya Kampuni	Kiasi cha Kemikali	
		Tani	Lita
2017	167	116,257.00	13,016,466.00
2018	184	1,534,064.00	11,247,555.00
2019	160	249,768.00	6,304,971.00
2020	87	96,062.44	4,256,161.00
2021	57	3,655.97	855,807.00
2022	94	11,389.00	5,711,266.00
2023	66	28,690.82	5,453,747.38
2024	72	7,080.50	2,954,009.50
2025	127	14,747.25	7,943,019.56

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Jedwali Na. 3.11 linaonesha kwa kipindi cha mwaka 2025, uingizwaji wa kemikali bashirifu uliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024, kuonesha mahitaji makubwa ya kemikali hizo hali iliyoenda sambamba na jitihada za kudhibiti uchepushaji.

3.5.1.1 Udhibiti wa Kemikali Bashirifu Kupitia Mifumo ya Kielektroniki

Mamlaka ilifanya ufuatiliaji kupitia Mifumo ya kieletroniki ya ndani ya Nchi na ya Kimataifa ambapo jumla ya matukio 78,809 yaliyoripotiwa duniani na kufanikiwa kuzuia uingizaji haramu wa Tani 734.1 na lita 69.769 za kemikali bashirifu. Kemikali zilizozuiliwa ni pamoja na sulphuric acid, toluene, acetic anhydride, Piperidone, pseudoephedrine, ephedrine, potassium permanganate na methyl ethyl ketone.

Jedwali Na. 3.12: Kiasi cha kemikali Bashirifu zilizozuiwa kuingia Nchini Mwaka 2017 hadi 2025

Mwaka	Tani	Lita
2017	250.1	-
2018	33.2	-
2019	43.6	-
2020	57.6	-
2021	120.3	-
2022	98.3	85
2023	159.3	1,000
2024	29.6	125
2025	734.1	69.769
Jumla	**1,526.1**	**1,279.769**

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Jedwali namba 3.12: Takwimu zinaonesha kwa kipindi cha mwaka 2025 kemikali bashirifu zilizozuiwa kuingia nchini zimeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024, hali inayohitaji juhudi za ufuatiliaji na udhibiti ili kuzuia uchepushwaji wa kemikali hizo kwa matumizi ya utengenezaji wa dawa za kulevya.

3.5.2 Ukaguzi wa Kemikali Bashirifu na Dawa Tiba zenye asili ya kulevya

Mwaka 2025 ulifanyika ukaguzi katika maeneo 135 yaliyopo mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Arusha, Tabora na Tanga kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa biashara ya kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya ili kubaini uchepushaji wa bidhaa hizo. Maeneo yaliyokaguliwa ni kampuni za kemikali

88, maduka ya dawa muhimu na famasi 31, bandari kavu tisa**,** kampuni nne za kusafirisha vifurushi na vituo vitatu vya forodha vya Namanga, Manyovu na Kibirizi.

Mamlaka kwa kushirikiana na GCLA na TMDA ilifanikiwa kukamata tani 31.76 na lita 813.5 za kemikali bashirifu, kilogramu 1.92 ya dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya Ketamine, gramu 444 za Flunitrazepam na vidonge 96 vya Codeine zilizokuwa zikisafirishwa kinyume cha sheria. Vile vile, ukaguzi ulibaini upotevu wa takribani tani saba za kemikali mbalimbali, ikiwemo kemikali bashirifu hali iliyoashiria uwepo wa uchepushwaji.   Hatua za kisheria zilichukuliwa kwa kampuni zilizohusika na makosa hayo.

Dawa tiba zenye asili ya kulevya aina ya codeine zilizokamatwa katika Shirika la usafirishaji wa vifurushi

3.6 Uchunguzi wa sampuli zilizodhaniwa kuwa Dawa za Kulevya

Mamlaka hufanya uchunguzi wa awali wa sampuli zinazodhaniwa kuwa Dawa za Kulevya katika maabara yake ya sayansi jinai ili kurahisisha ufuatiliaji na operesheni mbalimbali. Mwaka 2025 ulifanyika uchunguzi wa sampuli 587, kati ya hizo sampuli 44 zilibainika kuwa na dawa za kulevya ikiwemo heroin sampuli 14, bangi 12, norephedrine tisa, cocaine nne, MDMA tatu, methamphetamine moja na ketamine moja.

3.7 Mashauri ya Dawa za Kulevya

Mwaka 2025 mashauri ya dawa za kulevya 1,124 yalifunguliwa katika Mahakama mbalimbali nchini. Jumla ya mashauri 1,373 yalimalizika, yakiwemo mashauri yaliyofunguliwa miaka ya nyuma. Kati ya hayo Jamhuri ilishinda mashauri 1,058**,** ambapo watuhumiwa walitiwa hatiani na kuhukumiwa kutumikia vifungo mbalimbali.

3.8 Uteketezaji wa Dawa za Kulevya

Uteketezaji wa dawa za kulevya ulihusisha dawa za mashambani ambazo ni mirungi na bangi na dawa za viwandani ambazo ni heroin, cocaine na methamphetamine. Dawa hizo zilikuwa zimehifadhiwa kama vielelezo vya mashauri yanayoendelea mahakamani na yaliyotolewa hukumu. Kwa mashauri ambayo bado hayajamalizika, uteketezaji wa vielelezo vya mashauri yanayoendelea Mahakamani hufanyika kutokana na hatari ya kuharibika au kubadilika umbo na hufanyika kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sura ya 95.

Mwaka 2025 jumla ya tani 36.18 za dawa za kulevya ziliteketezwa. Mchanganuo wa dawa zilizoteketezwa ni tani 22.06 za bangi, mirungi tani 10.41, tani 2.65 za methamphetamine, tani 1.06 za heroin na gramu 326.95 za cocaine. Aidha, jumla ya ekari 3,512.25 za mashamba ya bangi na ekari 369.5 za mashamba ya mirungi ziliteketezwa.

3.9 Utaifishaji wa mali zilizotokana na Uhalifu wa Dawa za Kulevya

Katika kuendeleza hatua za kukabiliana na uhalifu wa dawa za kulevya, Mahakama kuu divisheni ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ilitoa maamuzi ya kutaifishwa kwa mali za watuhumiwa wa biashara ya dawa za kulevya zenye thamani zaidi ya Tsh. Bilioni Tatu na milioni mia tatu na nne (3,304,000,000/=). Mali zilizotaifishwa ni magari 16, nyumba 12, viwanja 11, pikipiki mbili (2) na jahazi moja (1).

Baadhi ya mali zilizotaifishwa

SURA YA NNE

KUPUNGUZA UHITAJI WA DAWA ZA KULEVYA (DEMAND REDUCTION)

4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea jitihada za Mamlaka kwa kushirikiana na wadau katika kupunguza uhitaji wa dawa za kulevya nchini. Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali hutoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ili jamii isijiingize katika matumizi ya dawa hizo. Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya hutolewa kupitia vyombo vya habari, machapisho, semina, makongamano, maonesho na maadhimisho mbalimbali ya kitaifa.

4.2 Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya yamekuwa yakihusisha makundi mbalimbali hususani vijana. Dawa aina ya bangi inaongoza kwa matumizi nchini. Aidha, dawa nyingine zinazotumika ni mirungi, cocaine pamoja na dawa za tiba zenye asili ya kulevya.

4.2.1 Matumizi ya Dawa za Kulevya kwenye vyakula

Matumizi ya Dawa za Kulevya kwenye vyakula ni kitendo cha kuchanganya dawa za kulevya au viambata vyake katika vyakula na vinywaji kwa lengo la kulevya. Katika siku za hivi karibuni matumizi ya bangi kwenye vyakula (edibles) yamebainika kwenye vyakula kama vile keki, biskuti, pipi, chokoleti na vinywaji mbalimbali. Hata hivyo, bangi imeendelea kutumika zaidi kwa njia ya kuvuta.

Ingawa baadhi ya watumiaji wanaweza kuona *edibles* ni salama zaidi taarifa ya Hali ya Dawa za Kulevya Duniani inaonesha kuwa matumizi hayo yana athari kubwa na za muda mrefu. Matumizi ya edibles husababisha kemikali ya THC kuingia mwilini kupitia tumbo na ini na kubadilishwa kuwa kemikali yenye nguvu zaidi (11-hydroxy-THC) ambayo inaweza kuwa na athari kubwa na za muda mrefu.

Pipi zenye bangi

Biskuti za bangi zilizokamatwa

4.2.2 Sheria Inasemaje kuhusu kuchanganya Dawa za Kulevya Kwenye Vyakula?

Kwa mujibu wa Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ni kosa la jinai kumwekea mtu dawa za kulevya kwenye chakula au kinywaji na kumfanya atumie dawa za kulevya bila kufahamu. Pia, ni kosa mtu kutumia dawa hizo kwa ridhaa yake. Kumwekea mtu dawa za kulevya kwenye vinywaji au chakula pasipo mtumiaji kujua kosa hilo halina dhamana na adhabu yake ni kifungo kisichopungua miaka 30 au faini isiyopungua shilingi milioni 50 au adhabu zote mbili kwa pamoja.

4.3 Sababu zinazochangia Matumizi ya Dawa za Kulevya

Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limeendelea kuisumbua jamii na taifa kwa ujumla. Hata hivyo, jitihada mbalimbali zimeendelea kufanyika ili kuiepusha jamii kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya. Sababu zinazochangia matumizi ya dawa za kulevya ni pamoja na:

a. Msukumo rika au Kufuata Mkumbo

Msukumo rika ni sababu kubwa inayochangia matumizi ya dawa za kulevya, hasa kwa vijana. Vijana hutumia muda mwingi na marafiki zao, hivyo huathiriwa kwa

urahisi na mienendo yao. Ikiwa kundi la marafiki linatumia dawa za kulevya, mtu anaweza kushawishika kutumia dawa hizo ili aonekane anakubalika katika kundi, asiwe wa tofauti au asidharauliwe.

b. Ukosefu wa Uelewa Sahihi Juu ya Madhara ya Dawa za Kulevya

Jamii ikiwa haina uelewa wa kutosha kuhusu athari za kiafya, kisaikolojia, kijamii na kiuchumi zinazotokana na matumizi ya dawa za kulevya ni rahisi kuingia katika matumizi ya dawa hizo. Watu hutafuta furaha, kukubalika na kujisahahulisha matatizo yao kwa kutumia dawa za kulevya na kujikuta wakiwa waraibu wa dawa hizo.

c. Upatikanaji wa Dawa za Kulevya

Upatikanaji rahisi wa dawa za kulevya, hasa zile zinazomea au kuzalishwa ndani ya nchi kama vile bangi na mirungi, ni sababu inayochochea matumizi ya dawa hizo. Hali hii hupunguza hofu ya matumizi kwa kuonekana ni kama mimea ya kawaida au sehemu ya tamaduni, hivyo kupuuza madhara yake. Uhalalishaji wa baadhi ya dawa za kulevya katika nchi jirani unarahisisha upatikanaji wa dawa hizo.

d. Ukuaji wa Sayansi na Teknolojia

Ukuaji wa sayansi na teknolojia umechangia kuongezeka kwa matumizi ya dawa za kulevya. Kupitia maendeleo ya sayansi, zimetengenezwa dawa mpya za kulevya zenye kemikali kali ambazo husababisha uraibu kwa haraka na kuongeza madhara kwa watumiaji. Baadhi ya dawa hizi hutengenezwa maabara bubu na hubadilishwa muundo na muonekano ili kuongeza ukali wa dawa hizo, jambo linaloshawishi watumiaji wengi. Aidha, maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano, hususan mitandao ya kijamii na intaneti, yamerahisisha biashara ya dawa za kulevya. Watu wanaweza kuwasiliana na wauzaji kwa siri na kuagiza dawa mtandaoni na kuzipata bila kutambulika (*dark webs*). Biashara ya kimtandao hutumia sarafu za kidigitali *“cryptocurrencies”,* hali hii imepunguza hofu ya kukamatwa na hivyo kuchochea matumizi.

e. Migogoro ya Kifamilia

Migogoro katika familia huchochea kukosekana maelewano, upendo na mshikamano unaopelekea msongo wa mawazo unaotokana na ugomvi wa mara kwa mara, talaka, unyanyasaji au kutelekezwa. Hali hii husababisha baadhi ya wanafamilia kutumia dawa za kulevya kama njia ya kukabiliana na changamoto hizo. Aidha, watoto wanaokulia katika familia zenye migogoro hukosa malezi bora

na baadhi kukimbilia mtaani hivyo hushawishika kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya kwa urahisi.

f. Kushindwa Kutumia Stadi za Maisha

Matumizi ya stadi za maisha ni silaha imara ya kukabiliana na changamoto za maisha ikiwemo ushawishi wa kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya. Stadi hizo huhusisha uwezo wa kufanya maamuzi sahihi, kujitambua, kudhibiti hisia, kukabiliana na msongo wa mawazo na kusema "hapana" kwa vishawishi ili kuishi maisha yenye maadili. Endapo mtu atashindwa kutumia stadi hizi huweza kushawishika kirahisi kuingia katika matumizi ya dawa za kulevya.

g. Imani potofu

Imani kuwa matumizi ya dawa za kulevya yana manufaa fulani, kama vile kuongeza nguvu za kufanya kazi, kupunguza msongo wa Mawazo na kuongeza ujasiri huchochea matumizi ya dawa za kulevya katika jamii. Imani hizi huwafanya watu kuanza kutumia dawa hizo bila kutambua kuwa zina madhara makubwa ya kiafya na kijamii. Aidha, baadhi ya watu huamini kuwa kutumia dawa za kulevya kwa kiwango kidogo au mara chache hakuleti madhara. Mtazamo huu huwafanya waendelee kuzitumia taratibu hadi kufikia hatua ya uraibu.

h. Matumizi yasiyo sahihi ya dawa tiba zenye asili ya kulevya

Baadhi ya dawa tiba kama vile dawa za kupunguza maumivu makali, dawa za usingizi au za kutibu changamoto za akili huwa na kemikali zinazoweza kusababisha uraibu endapo zitatumiwa bila ushauri sahihi wa kitaalamu. Watu wanapoanza kutumia dawa hizi kwa lengo la matibabu, na kuamua kuendelea kuzitumia kupita kiasi hadi kufikia uraibu. Matumizi ya dawa hizi bila kufuata maagizo ya daktari, kama vile kuongeza dozi, kutumia kwa muda mrefu kuliko inavyoshauriwa huleta madhara kwa mtumiaji kama yanayotokana na dawa za kulevya.

i. Magonjwa ya Akili

Watu wenye matatizo ya afya ya akili kama vile msongo wa mawazo (depression), wasiwasi mkubwa, sonona na maradhi mengine ya akili mara nyingi hukumbwa na maumivu ya kihisia na kisaikolojia. Kutokana na hali hiyo, baadhi yao huamua kutumia dawa za kulevya kama njia ya kukabiliana na matatizo hayo.

j. Kurithi Vinasaba vya Uraibu wa Dawa za Kulevya

Utafiti wa kisayansi umeonesha kuwa baadhi ya watu wana urithi wa vinasaba unaowafanya wawe katika hatari zaidi ya kupata uraibu wanapojaribu kutumia

dawa za kulevya. Hii inamaanisha kwamba familia zenye historia ya uraibu wa dawa za kulevya zina uwezekano mkubwa wa kuwa na vizazi vinavyopata uraibu pia.

4.4 Madhara ya Matumizi ya Dawa za Kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya ni hatari kwani huweza kusababisha madhara ya kiafya, kijamii, kiuchumi, kisiasa na kimazingira. Madhara hayo yameelezewa kwa kina kama ifuatavyo;

4.4.1 Kiafya

Matumizi ya dawa za kulevya kwa binadamu yana madhara makubwa ambayo huathiri mwili, akili na ustawi wa jamii. Dawa hizo husababisha magonjwa ya moyo, figo, ini, ngozi, shinikizo la damu, kiharusi pamoja na uraibu unaosababisha kupata arosto kali. Aidha, husababisha changamoto za afya ya akili, kupoteza kumbukumbu, kupungua uwezo wa kufikiri, kukosa usingizi na kushindwa kufanya maamuzi sahihi. Pia huongeza hatari ya kupata magonjwa ambukizi kwa wajidunga kama vile kifua kikuu, virusi vya UKIMWI na homa ya ini B na C. Aidha, matumizi ya dawa za kulevya huweza kusababisha saratani na matatizo katika mfumo wa uzazi hasa utasa, ugumba, upungufu wa nguvu za kiume, kuvurugika kwa mfumo wa hedhi, kuharibika kwa mimba, kuzaliwa kwa watoto njiti, watoto wenye ulemavu na wenye vinasaba vya uraibu. Vile vile, husababisha vifo vya ghafla hasa mtumiaji anapozidisha kiasi cha dawa za kulevya (overdose). Kwa ujumla madhara haya huweza kutofautiana kulingana na umri, kiasi cha dawa, aina ya dawa na muda ambao mtu ametumia dawa hizo.

4.4.2 Kijamii

Matumizi ya dawa za kulevya kwenye jamii huweza kuathiri mahusiano ya kifamilia kutokana na migogoro ya mara kwa mara inayopelekea kuvunjika kwa ndoa na watoto kukosa malezi bora. Watumiaji wanaweza kujihusisha na vitendo vya kihalifu kama wizi, unyang'anyi, ubakaji, ukatili wa kijinsia, utapeli, utekaji na biashara haramu ili kupata fedha za kununulia dawa hizo. Vilevile, wafanyabiashara wa dawa hizo hujihusisha na vitendo vya utekaji, mauaji, uuzaji wa silaha haramu, usafirishaji haramu wa binadamu na kuondoa utulivu na usalama. Jamii isiyojihusisha na dawa za kulevya huweza kuambukizwa virusi vya UKIMWI, homa ya ini na kifua kikuu kutoka kwa waraibu waliothirika na magonjwa hayo na kuongeza maambukizi hayo kwenye jamii. Aidha, uharibifu wa miundombinu, mali, ulemavu wa kudumu na vifo vinavyotokana na ajali ni matokeo ya matumizi ya dawa za kulevya.

\Wanafunzi wanaojihusisha na matumizi ya dawa hizo huathirika kitaaluma, utovu wa nidhamu na vitendo vya kihalifu vinavyopelekea kushindwa kutimiza malengo

yao. Pia, waraibu wa dawa za kulevya hukumbana na changamoto ya unyanyapaa kutoka kwa baadhi ya wanajamii hali ambayo inazidisha ukubwa wa tatizo na kupelekea wale walioacha kurudi kwenye matumizi ya dawa hizo.

4.4.3 Kiuchumi

Matumizi na biashara ya dawa za kulevya husababisha madhara ya kiuchumi kwa mtu binafsi, familia na taifa kwa ujumla. Kwa mtu binafsi hupelekea kupoteza ajira, kupungua kwa ufanisi kazini na matumizi makubwa ya fedha kwa ajili ya kununua dawa hizo badala ya kuwekeza kwenye shughuli za kiuchumi kwa ajili ya kuongeza kipato. Kwa upande wa familia hali hii huleta umasikini kutokana na wizi na gharama za matibabu kwa waraibu. Kwa taifa matumizi na biashara ya dawa hizo hupelekea kupungua kwa nguvu kazi, kuongezeka kwa vitendo vya rushwa, utakatishaji fedha, mfumuko wa bei, serikali huingia gharama za matibabu kwa watu wenye uraibu na kuendesha operesheni ili kudhibiti biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

4.4.4 Kisiasa/Kidiplomasia

Biashara ya dawa za kulevya hudhoofisha utawala wa sheria na kuchochea migogoro ya kisiasa inayoweza kuchangia machafuko. Aidha, fedha haramu zinazotokana na biashara hiyo huweza kufadhili kampeni za kisiasa ili kuwapata viongozi watakaolinda maslahi ya wafanyabiashara ya dawa za kulevya. Kidiplomasia kukithiri kwa biashara ya dawa za kulevya huchafua taswira ya nchi na kutoaminika hivyo kuleta misuguano baina ya mataifa na huweza kusababisha nchi kuwekewa vikwazo au masharti na nchi nyingine.

4.4.5 Kimazingira

Kilimo cha bangi na mirungi huhusisha ukataji wa miti, hali hii husababisha uharibifu wa misitu, kuongezeka kwa mmomonyoko wa udongo na kupotea kwa bayoanuwai. Pia, matumizi ya kemikali kwa ajili ya kukuza mimea na kuua wadudu huathiri rutuba ya udongo na ikolojia ya maeneo yanakofanyika kilimo hicho. Mchakato wa kutengeneza dawa za kulevya kwenye maabara bubu hutumia kemikali zinazotupwa hovyo kwenye mito, maziwa, mitaro na kwenye ardhi ambazo husababisha uchafuzi wa mazingira.

Vile vile watumiaji wa dawa za kulevya kwa njia ya kujidunga hutupa hovyo vifaa vya kujidungia kama vile sindano kwenye maeneo ya wazi yanayotumika kwa shughuli za kijamii. Moshi unaotokana na uvutaji wa bangi na dawa nyingine za kulevya huchafua hewa na kuhatarisha afya za watu wasiotumia dawa hizo.

Shamba la bangi

4.4.6 Unyanyapaa

Waraibu wa dawa za kulevya wanapitia changamoto za kunyanyapaliwa na jamii kwa kuonekana kama wahalifu, wavivu na wasio na maadili. Hali hii husababisha kukosa kazi, kufukuzwa shuleni, vyuoni, kutoaminika, kukosa haki zao mbalimbali na kupewa majina mabaya. Baadhi ya wanajamii huwahukumu waraibu hao badala ya kuwasaidia, jambo linalopelekea kutotafuta matibabu, kuathirika kwa afya ya akili na kuendelea kutumia ya dawa za kulevya. Hivyo jamii inapaswa kufahamu kwamba uraibu ni ugonjwa unaoweza kutibika.

4.5 Jitihada zilizofanyika katika Kupunguza Uhitaji wa Dawa za Kulevya

4.5.1 Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani

Siku hii huadhimishwa kila mwaka tarehe 26 Juni duniani kote ikiwa na lengo la kuhamasisha jamii kushiriki katika mapambano dhidi ya tatizo la dawa za kulevya. Mwaka 2025 maadhimisho hayo yalifanyika kitaifa jijini Dodoma kuanzia tarehe 24 hadi 26 Juni, katika ukumbi wa Jakaya Kikwete. Mgeni rasmi alikuwa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyewakilishwa na Mh. Kasssim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika siku hiyo wadau wanaojihusisha na udhibiti wa dawa za kulevya walishiriki kuonesha kazi zao ikiwemo kutoa elimu kwa jamii ambapo takriban watu 145,000 walipata elimu na huduma nyingine.

Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mh. Kasssim Majaliwa Majaliwa (Mb) akiwa Pamoja na viongozi wengine katika Siku ya Kupiga Vita Dawa za Kulevya Duniani, jijini Dodoma

4.5.2 Mafunzo juu ya Mwongozo wa Utoaji Elimu

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na *Colombo Plan*-DAP ilitoa mafunzo maalum kwa walimu na Asasi za kiraia (Training on Trainers) kwenye mikoa ya Tanga na Arusha lengo likiwa kuwajengea uwezo washiriki waweze kutoa elimu sahihi juu ya madhara ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya kwa makundi mbali mbali ya jamii. Jumla ya washiriki 151 walipatiwa mafunzo hayo.

4.5.3 Elimu kwenye Taasisi za Elimu

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa na Mamlaka kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari pamoja na wanavyuo wa vyuo vikuu na vya kati nchini. Takribani wanafunzi 4,650,477 walipata elimu hiyo katika shule na vyuo mbalimbali nchini -ikiwemo, Chuo Kikuu cha Tumaini (Dar es Salaam na Arusha), Mzumbe - (Dar es Salaam, Mbeya na Morogoro), Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere - Dar es Salaam, Chuo kikuu cha Dodoma, Sokoine, Chuo kikuu cha Kiislam - Morogoro, Ardhi - Dar es Salaam, Chuo kikuu Huria, Kairuki, Chuo kikuu cha Katoliki CUOM-Mbeya, IFM (Dar es Salaam na Mwanza), Vyuo vya Ualimu Dakawa na Korogwe, Chuo cha Utumishi-Tanga, vyuo vya ufundi VETA, Taasisi za Uhasibu – Arusha na Mbeya, Chuo cha Utalii Arusha (NCT), Chuo kikuu cha

Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Ustawi wa Jamii Dar es Salaam. Baadhi ya shule za sekondari zilizopata elimu ni Kilakala, Mzumbe, Kibaha, Hassanali Damji, Pangani, Tandika, Mbagala, Butiama, Mitengo, Naliendele, Kisimiri, Lesinoni na Shule ya Msingi Greenvalley, Zachas, Chikongola na Misufi.

Elimu ikitolewa kwa wanafunzi

4.5.3.1 Mafunzo Kwenye Wiki ya Utambulisho Vyuoni (Orientation Week)

Katika kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya nchini Mamlaka ilitekeleza maelekezo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ya kutoa elimu kinga juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza kwenye vyuo vikuu na vyuo vya kati vyote nchini. Lengo la programu hii maalum ilikuwa ni kuwaepusha vijana hao kujihusisha na matumizi na biashara hiyo haramu. Jumla ya wanachuo 42,850 wa vyuo 59 vilipatiwa elimu hiyo.

4.5.4 Vyombo vya Ulinzi na Usalama

Biashara na matumizi ya dawa za kulevya ni uhalifu unaohitaji nguvu ya pamoja ya vyombo vya ulinzi na usalama. Mwaka 2025 Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya kwa vyombo hivyo ili kuongeza nguvu ya mapambano dhidi ya tatizo hilo. Askari wa Jeshi la Magereza 812 na wafungwa 2,408 katika mikoa ya Mbeya, Rukwa, Mtwara na Mwanza, Askari wa jeshi la Polisi 70 na 36 wa jeshi

la Zimamoto na Uokoaji katika mkoa wa Arusha walipata elimu. Lengo likiwa ni kuwajengea uwezo wa kukabiliana na tatizo hilo katika majukumu yao ya kila siku.

4.5.5 Majukwaa ya Kitaaluma

Mamlaka ilitoa elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya katika mikutano ya kitaaluma inayofanyika nchini kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya tatizo la dawa za kulevya na pia kuwahamasisha wanataaluma kutumia elimu hiyo kupambana na dawa za kulevya katika mazingira yao ya kila siku. Mikutano ya kitaaluma iliyopata elimu juu ya dawa za kulevya ni pamoja Chama cha Wanasaikolojia Tanzania (TAPA) ambapo wanasaikolojia wapatao 250 walipata elimu hiyo.

4.5.6 Wadau wanaojihusisha na kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeweza kutoa elimu ya Udhibiti wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa wadau takribani 700 wa kemikali bashirifu. Uelimishaji huu ulifanyika kwa ushirikiano na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA). Waliopatiwa mafunzo hayo ni pamoja na waingizaji wa kemikali, watumiaji wa kemikali, maafisa wa vituo vya forodha vya mipakani, wajasiriamali, wasimamizi wa shughuli za kemikali, madereva wanaosafirisha kemikali, wakaguzi wa dawa tiba pamoja na wamiliki na wasimamizi wa maduka ya dawa tiba.

4.5.7 Vyombo ya Habari

Elimu imekuwa ikitolewa kwenye vipindi mbalimbali vya uelimishaji kuhusu tatizo la dawa za kulevya kupitia runinga, redio ikiwemo redio za kijamii, magazeti, majarida, blogu na mitandao ya kijamii nchini. Vyombo hivyo ni pamoja na ITV, Azam TV, TBC, Clouds TV, Channel Ten, Star TV, na vituo vya redio kama vile TBC FM, Radio One, Capital Radio na Clouds Radio.

Aidha, Mamlaka imekuwa ikitumia studio yake, tovuti, kurasa za Instagram, Mtandao wa X, Facebook, You Tube na simu ya bure 119 kufikisha elimu ya dawa za kulevya kwenye jamii. Inakadiriwa watu milioni 15.3 walifikiwa na elimu hiyo.

4.5.8 Asasi za Kiraia

Asasi za kiraia zimekuwa na mchango mkubwa kuisaidia serikali kufikisha elimu ya dawa za kulevya kwenye jamii. Katika mwaka 2025 asasi za kiraia 75 ziliweza kufikia watu wapatao 4,835,489, wanaume 1,712,290 na wanawake 3,123,199 kwa kutumia mbinu mbalimbali. (rejea kiambata cha I)

4.5.9 Taasisi za Serikali

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa askari wanafunzi na maafisa 494 wa Wakala wa Uhifadhi wa Misitu (TFS – Mwanza na Katavi), Maafisa wa TAKUKURU na Waendesha mashtaka 50 mkoani Mwanza, Walimu wa Sayansi 730, Wathibiti Ubora Elimu wa kanda 13, Maafisa Wizara ya Elimu, Taasisi ya Watu Wazima na TAMISEMI 30, Mahakimu 20 na timu ya taifa ya wakimbiza Mwenge wa Uhuru.

4.5.10 Maadhimisho na Matamasha

Maadhimisho ya kitaifa yaliyotumika katika kutoa elimu ni pamoja na Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) Mkoani Dar es salaam, Maonesho ya siku ya wakulima (Nanenane) mkoani Dodoma, Uzinduzi wa Mbio za Mwenge uliofanyika Mkoani Pwani, Maadhimisho ya wiki ya vijana yanayoambatana na Kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru na Kumbukizi ya Kifo cha Mwalimu Nyerere Mkoani Mbeya. Takribani watu 250,000 wapatiwa elimu katika matukio hayo.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe. Ummy Nderiananga akiwa katika banda la Mamlaka wakati wa Maonesho ya 49 ya Biashara ya Kimataifa (Saba Saba) jijini Dar es salaam

4.5.11 Watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani

Watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani wapo kwenye hatari kubwa ya kuingia katika matumizi na biashara ya dawa za kulevya. Katika kukabiliana na hali hiyo inahitajika familia na jamii kuwekeza katika elimu, malezi bora na huduma za kisaikolojia. Hii itasaidia kupunguza uwezekano wa watoto kuingia kwenye matumizi ya dawa za kulevya.

Serikali kwa kushirikiana na Shirika la SOS Children's Villages ilianza kutoa huduma za kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani mwaka 2025. Huduma hii ilitolewa katika makao ya watoto kwenye mikoa ya Mwanza, Dar es Salaam na Dodoma. Jumla ya watoto 599 walipata elimu, kati ya hao watoto 397 walifanyiwa uchunguzi ambapo watoto 22 (wavulana 19 na wasichana 3) walibainika kuwa na viashiria vya matumizi ya dawa za kulevya hususan bangi. Hali hii inaashiria uwepo wa matumizi ya dawa za kulevya kwa watoto ambapo serikali inatekeleza mpango maalum wa kukabiliana na tatizo hili.

Jedwali Na: 4.1: Idadi ya Watoto Waliopewa Elimu na Kufanyiwa Vipimo

Na.	Jina la Makao	Mkoa	Waliopewa Elimu		Waliopimwa		Waliobainika Kutumia Bangi	
			Me	**Ke**	**Me**	**Ke**	**Me**	**Ke**
1.	Kikombo	Dodoma	59	11	50	11	2	3
			70		**61**		**5**	
2.	Kurasini	Dar-es- Salaam	50	15	19	5	11	0
			65		**24**		**11**	
3.	Yatima Group Trust Fund		19	11	19	11	1	0
			45		**30**		**1**	
4.	Child in the Sun		50	0	40	0	1	0
			50		40		1	
5.	Umra Orphanage Centre		11	19	9	15	0	0
			30		**24**		**0**	
6.	Youth Counselling Centre		45	15	17	17	2	0
			50		**3**		**2**	

Na.	Jina la Makao	Mkoa	Waliopewa Elimu		Waliopimwa		Waliobainika Kutumia Bangi	
7.	Upendo Daima	Mwanza	7	25	7	25	0	0
			32		**32**		**0**	
8.	Kiota Women Health and Development (KIWOHEDE)		01	25	1	11	0	0
			26		**12**		**0**	
9.	Watoto wa Afrika		59	23	35	17	0	0
			82		**52**		**0**	
10.	Hisani Orphanage Centre		68	38	28	17	0	0
			106		**45**		**0**	
11.	Tanzania Children Rescue Centre		38	5	38	5	2	0
			43		**43**		**2**	
Jumla			**599**		**397**		**22**	

4.5.12 Makundi Mengine yaliyoelimishwa

Elimu juu ya tatizo la dawa za kulevya ilitolewa kwa watu 13,700 ikihusisha waraibu wa dawa za kulevya, vijana wanaofanya biashara ya usafirishaji (bodaboda), Uelimishaji katika Taasisi za Dini. Watoa huduma kwenye vituo vya afya, wajawazito, mama wanaonyonyesha, waraibu wanaopata huduma kwenye vituo vya MAT, ndugu wa waraibu, waelimisha rika na wafanyabiashara.

Elimu mtaani

SURA YA TANO

KUPUNGUZA MADHARA YANAYOTOKANA NA MATUMIZI YA DAWA ZA KULEVYA (HARM REDUCTION)

5.1 Utangulizi

Matumizi ya dawa za kulevya yameendelea kuwa tishio kubwa kwa afya na ustawi wa jamii nchini na duniani. Upunguzaji wa madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya ni moja ya nguzo muhimu iliyothibitishwa kisayansi katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya. Hata hivyo, pamoja na jitihada za ukamataji wa wafanyabiashara wa dawa za kulevya na utoaji wa elimu sahihi kwa umma, baadhi ya jamii zimeendelea kuathirika na matumizi ya dawa hizo.

Sura hii inaelezea jitihada zilizofanyika katika kupunguza madhara yanayotokana na matumizi ya dawa za kulevya kwa lengo la kuimarisha afya na ustawi wa jamii. Katika kutekeleza jitihada hizo, serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetoa matibabu na huduma za utengamao katika vitengo vya afya ya akili, tiba saidizi kwa kutumia dawa na unasihi (MAT), tiba kwenye nyumba za upataji nafuu na huduma za kijamii na rufaa kupitia Asasi za kiraia. Aidha, waraibu wanaojidunga hupatiwa huduma maalum ya kuzuia maambukizi ya magonjwa yanayoambukiza kwa njia ya damu (Needle and Syringe Program-NSP). Huduma nyingine zinazotolewa ni urudishaji na ujumuishi wa waraibu katika jamii.

5.2 Huduma ya matibabu ya Uraibu katika Vitengo vya Afya ya Akili

Serikali imeendelea kusimamia na kuboresha utoaji wa tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya katika vitengo vya afya ya akili vilivyo katika hospitali za rufaa, mikoa na wilaya nchini. Kwa kipindi cha mwaka 2025, jumla ya waraibu 62,926 wa dawa mbalimbali za kulevya walipatiwa huduma hiyo, kati ya hao wanaume 46,464 na wanawake 16,462. Watu wenye uraibu waliotibiwa katika vituo hivyo walibainika kuathirika na pombe, bangi, mirungi, heroin na cocaine. Aidha, baadhi yao walibainika kutumia dawa tiba zenye asili ya kulevya kama vile Valium, Pethidine na Tramadol. Watu wenye uraibu walipatiwa matibabu ya dawa, unasihi pamoja na rufaa mbalimbali kutokana na changamoto walizokuwa nazo.

Jedwali Na.5.1: Idadi ya Watu wenye Uraibu waliopata Tiba kwenye Vitengo vyaAfya ya Akili Nchini kwa Mwaka 2025

Kituo (Mkoa)	Wanaume	Wanawake	Jumla
Muhimbili	8,231	23,232	31,463
Arusha	290	1,653	1,943
Dar es Salaam (Mwananyamala, Temeke na Amana)	1,429	10,743	12,172
Dodoma	669	545	1,214
Geita	130	130	260
Iringa	75	105	180
Kagera	203	322	525
Katavi	120	95	215
Kigoma	693	635	1,328
Kilimanjaro	749	832	1,581
Lindi	142	113	255
Manyara	130	251	381
Mara	117	153	270
Mbeya	214	271	485
Morogoro	605	531	1,136
Mtwara	163	142	305
Mwanza	360	1,604	1,964
Njombe	98	109	207
Pwani	417	2,895	3,312
Rukwa	144	108	252
Ruvuma	269	255	524
Shinyanga	179	161	340
Simiyu	151	140	291
Singida	77	148	225
Songwe	168	193	361
Tabora	294	221	515
Tanga	345	877	1,222
Jumla Kuu	**16,462**	**46,464**	**62,926**

Chanzo: Wizara ya Afya (2025)

Jedwali namba 5.1 linaonesha idadi ya watu wenye uraibu waliopata tiba kwenye vitengo vya afya ya akili. Idadi ya waliotibiwa Muhimbili inahusisha wale waliopewa rufaa kutoka vitengo vingine vya afya akili nchini. Watu wenye uraibu wa mkoa wa Dar es Salaam walihudumiwa kwenye vitengo vya afya ya akili vya Mwananyamala, Temeke na Amana.

5.3 Huduma ya Tiba Saidizi kwa Kutumia Dawa na Unasihi (Medically Assisted Therapy-MAT)

Matumizi ya dawa za kulevya, hususan za jamii ya afyuni kama heroin na dawa za tiba zenye asili ya kulevya kama Tramadol, Pethidine, Morphine, Fentanyl na nyinginezo, yameendelea kusababisha madhara makubwa kwa jamii. Dawa za afyuni zinachangia zaidi katika kusababisha vifo vya ghafla pamoja na maambukizi ya virusi vya UKIMWI, homa ya ini na kifua kikuu duniani. Serikali imeendelea kuimarisha huduma za MAT ambayo ni maalum kwa matibabu ya uraibu wa dawa za kulevya za jamii ya afyuni hususan heroin. Hadi kufikia mwaka 2025, MAT ilitoa dawa tiba aina ya Methadone na Suboxone (Buprenorphine na Naloxone) pamoja na huduma ya unasihi bila malipo katika vituo maalum chini ya uangalizi wa watoa huduma. Asasi za kiraia huibua waraibu kutoka mitaani na kuwapa mafunzo pamoja na unasihi kabla ya kupata rufaa za kwenda katika vituo vya MAT.

Hadi kufikia Desemba 2025, huduma za MAT zilitolewa kwenye vituo 18 kwa waraibu 18,048 ambapo kati ya hao 17,301 walikuwa wanaume na 747 wanawake. Takwimu zinaonesha kwamba idadi ya waraibu wapya wanaosajiliwa imepungua kutoka 2,060 mwaka 2024 hadi 840 mwaka 2025. Hali hii inatokana na serikali kuimarisha udhibiti wa upatikanaji wa dawa za kulevya aina ya heroin, na utoaji wa elimu sahihi kwa umma dhidi ya matumizi na biashara ya dawa za kulevya pamoja na kupungua kwa uzalishaji wa dawa hiyo nchini Afghastan

Ushuhuda kutoka kwa wanufaika wa huduma za MAT

Jedwali namba.5.2: Idadi ya watu wenye uraibu waliohudumiwa kwenye vituo vya MAT kuanzia mwaka 2011 hadi 2025

S/N	Kituo	Mahali	Mwaka wa Kuanzishwa	Mkoa	Jumla	Wanaume	Wanawake
1.	MAT Muhimbili	Hospitali ya Taifa ya Muhimbili	2011	Dar es Salaam	3,960	3,802	158
2.	MAT Mwananyamala	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mwananyamala	2012		4,051	3,788	263
3.	MAT Temeke	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Temeke	2014		3,630	3,521	109
4.	MAT Kigamboni	Hospitali ya Wilaya ya Vijibweni, Kigamboni	2021		110	102	8
5.	MAT Mbeya	Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Mbeya	2017	Mbeya	560	541	19
6.	MAT SekouToure	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Sekou Toure	2018	Mwanza	865	822	43
7.	MAT Itega	Hospitali ya Rufaa ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe	2019	Dodoma	658	630	28
8.	MAT Itega	Hospitali ya Rufaa ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe	2019		658	630	28
9.	MAT Bagamoyo	Hospitali ya Rufaa ya Wilaya ya Bagamoyo	2020	Pwani	850	836	14
10.	MAT Kibaha	Hospitali ya Rufaa ya Wilaya ya Tumbi, Kibaha	2020		573	566	7
11.	MAT Bombo	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa, Bombo	2020	Tanga	1,357	1,323	34
12.	MAT Mount Meru	Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mount Meru	2021	Arusha	869	825	44
13.	MAT Tunduma	Kituo cha Afya Tunduma	2021	Songwe	205	199	6
14.	MAT Kihonda	Zahanati ya Gereza la Kihonda	2021	Moro-goro	360	346	14
Jumla Kuu					**18,048**	**17,301**	**747**

Chanzo: Kanzi Data DCEA 2025

Mnufaika wa Methadone akipata huduma kwenye kituo cha MAT

Serikali imefanikiwa kuongeza vituo viwili vya MAT katika wilaya za Muheza mkoani Tanga na Chalinze mkoa wa Pwani. Aidha, serikali kwa kushirikiana na Mfuko wa Dunia (Global Fund), imekamilisha ujenzi wa vituo vinne vipya vya MAT katika Halmashauri za Moshi mkoani Kilimanjaro, Manispaa ya Kahama, Shinyanga Mjini na Mkuranga mkoa wa Pwani.

Kituo kipya cha MAT Chalinze mkoa wa Pwani

5.4 Huduma ya Kupunguza Magonjwa Ambukizi kwa Wajidunga (Needle and Syringe Program-NSP)

Wajidunga wa dawa za kulevya wamebainika kuwa na kiwango kikubwa cha maambukizi ya magonjwa yanayoenezwa kwa njia ya damu hususan VVU na homa ya ini aina B na C. Mkakati wa kupunguza usambazaji wa maradhi hayo kwenye jamii huhusisha utoaji elimu juu ya udungaji salama ambapo mabomba ya sindano hutolewa na yaliyotumika hukusanywa kuepusha kutumika tena au kuwachoma wasiotumia dawa hizo. Huduma hii hutolewa bure kwa wajidunga ambapo asasi za kiraia hutembelea vijiwe vya wajidunga (outreach service) na kuwapatia elimu na vifaa husika. Vilevile, asasi hizo hutumia fursa hiyo kufanya unasihi shawishi na utoaji wa rufaa kwa waraibu kujiunga na tiba za uraibu. Katika kipindi cha mwaka 2025, jumla ya walengwa 4,707 walifikiwa na huduma hii katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mwanza, Pwani na Morogoro.

5.5 Huduma katika Nyumba za Upataji Nafuu (Sober Houses)

Nyumba hizi zinamilikiwa na asasi za kiraia au watu binafsi kwa lengo la kutoa huduma za upataji nafuu kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya. Mhusika hupatiwa huduma kwa kipindi cha miezi minne au zaidi. Afua zinazotolewa katika nyumba hizi ni tiba kwa kutumia hatua 12 za upataji nafuu, unasihi, msaada wa kisaikolojia na kijamii, tiba kazi pamoja na matibabu ya kimwili na akili kwa kutumia wataalamu wa nje au ndani ya nyumba. Serikali huzisimamia na kuziratibu kwa kutumia *Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Nyumba za Upataji Nafuu Tanzania Bara.*

Kuanzia mwaka 2021 hadi mwaka 2025 jumla ya watu wenye uraibu 17,535 walihudumiwa katika nyumba za upataji nafuu, wanawake wakiwa asilimia 6.4 na wanaume asilimia 93.6**.** Kwa mwaka 2025 jumla ya watu wenye uraibu 4,451 walihudumiwa ambapo wanawake walikuwa 378 na wanaume 4,073**. *(rejea jedwali namba 5.3 na kiambata cha II.)***

Jedwali namba 5.3: Idadi ya watu wenye uraibu waliohudumiwa katika Nyumba za Upataji Nafuu Mwaka 2021 hadi 2025- Tanzania Bara

Mwaka		2021	2022	2023	2024	2025	Jumla
Idadi	Me	2,949	3,056	3,283	3,042	4,073	**16,403**
	Ke	160	124	205	265	378	**1,132**
Jumla		**3,109**	**3,180**	**3,488**	**3,307**	**4,451**	**17,535**

Chanzo: Taarifa kutoka Nyumba za Upataji Nafuu (2025)

Wakazi wa 'Sober house' ya wanawake

Idadi ya watu wenye uraibu waliohudumiwa katika nyumba za upataji nafuu imeendelea kuongezeka kuanzia mwaka 2021 hadi 2025. Ongezeko hilo linachangiwa na kuongezeka kwa uelewa juu ya huduma zinazotolewa katika nyumba za upataji nafuu, kuongezeka kwa nyumba za upataji nafuu, kupungua kwa unyanyapaa, kuimarika kwa udhibiti wa dawa za kulevya uliopelekea kuadimika kwa dawa hizo mtaani na uboreshwaji wa huduma katika nyumba hizo.

Ramani ya Tanzania ikionesha Vituo vya Tiba na Utengamao



5.6 Huduma za Kisaikolojia

Changamoto za kisaikolojia na kijamii ni moja ya sababu zinazochangia kuingiza watu kwenye uraibu wa dawa za kulevya pamoja na kushindwa kupata nafuu kwa haraka miongoni mwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya. Kutokana na hilo, Serikali imeendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri na unasihi katika vitengo vya afya ya akili katika hospitali za rufaa, mikoa na wilaya. Aidha, Asasi za kiraia na mashirika ya kimataifa yamekuwa yakitoa huduma za msaada wa kisaikolojia na kijamii kwa watumiaji wa dawa za kulevya na jamii ya waathirika wa dawa hizo. Walengwa hupatiwa huduma hizo na wataalamu waliobobea katika utoaji wa huduma za kisaikolojia, mathalani tiba za mabadiliko ya kitabia, huduma za ushauri na unasihi kwa familia, tathmini za afya ya akili.

5.7 Faida za Matibabu kwa watu wenye Uraibu wa Dawa za Kulevya

Utoaji wa huduma za matibabu kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya umeonesha manufaa ya moja kwa moja kwa waraibu na jamii. Yafuatayo ni manufaa yanayotokana na huduma hizo:-

i. Kupata nafuu ya uraibu kwa watumiaji wa dawa za kulevya.
ii. Kutibiwa magonjwa mengine yanayotokana na uraibu wa dawa za kulevya na hivyo kuimarika kwa afya ya mwili na akili.
iii. Kupunguza maambukizi ya VVU/UKIMWI, kifua kikuu, homa ya ini B na C, magonjwa ya zinaa pamoja na vifo vitokanavyo na kuzidisha kiasi cha matumizi ya dawa za kulevya (overdose).
iv. Kupunguza unyanyapaa kwa waraibu wa dawa za kulevya katika jamii.
v. Kurudisha nguvu kazi iliyopotea.
vi. Kupunguza uhalifu na uvunjifu wa amani katika jamii.
vii. Kuwarejesha watu waliokuwa na uraibu kwenye familia zao.
viii. Kupunguza matumizi na biashara ya dawa za kulevya na uchepushwaji wa dawa tiba zenye asili ya kulevya.

5.8 Asasi za Kiraia zilizowezeshwa na Serikali mwaka 2025

Serikali imeendelea kupanua wigo wa ushiriki katika udhibiti wa dawa za kulevya kwa kuzishirikisha Asasi za kiraia zinazofanya kazi za udhibiti wa dawa za kulevya. Katika kutekeleza jukumu hili Serikali imeratibu na kuziwezesha Asasi 17 zinazopatikana katika mikoa mbalimbali nchini.

Miongoni mwa majukumu yanayotekelezwa na Asasi hizi kutoa elimu, kuwaibua na kuwaunganisha kwenye matibabu watu wenye uraibu. Taasisi hizi zinatekeleza majukumu yake kwa kufuata miongozo ya serikali.

SURA YA SITA

USHIRIKIANO WA KITAIFA, KIKANDA NA KIMATAIFA KATIKA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

6.1 Utangulizi

Tatizo la dawa za kulevya ni uhalifu wa kupangwa unaovuka mipaka ambao huendeshwa na mitandao ya kihalifu iliyopo maeneo mbalimbali duniani. Mkakati huu unaelezea jinsi serikali ilivyoshirikiana na wadau mbalimbali kitaifa, kikanda na kimataifa katika kukabiliana na tatizo hilo.

6.2 Ushirikiano wa Kitaifa

Mamlaka ilishirikiana na Taasisi nyingine katika utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni pamoja na utoaji elimu, utoaji wa huduma za tiba na utengamao kwa watu wenye uraibu wa dawa za kulevya, kufanya operesheni na ukamataji, udhibiti wa uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya, uendeshaji wa mashtaka na maboresho ya sheria.

Mamlaka ilishirikiana na wadau mbalimbali nchini ikiwemo wizara zenye dhamana ya Afya, Elimu, Mambo ya Ndani, Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, TAMISEMI, Sheria na Katiba, Fedha, Kilimo, Ujenzi, Maendeleo ya Vijana, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Watu Wenye Mahitaji Maalum na Habari, Sanaa na Michezo. Vilevile, ilishirikiana na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Zanzibar, Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Idara ya Usalama wa Taifa, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Idara ya Uhamiaji, TANAPA, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shirika la Posta Tanzania, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mamlaka ya Anga (TCAA) pamoja na Baraza la Famasi.

Aidha, Mamlaka na Taasisi za udhibiti ilishirikiana na Sekta binafsi kudhibiti uchepushwaji wa kemikali bashirifu na dawa tiba zenye asili ya kulevya kwa kutoa mafunzo na kubadilishana taarifa. Katika kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika ushirikiano huo, Rasimu ya Katiba ya uanzishwaji wa jumuiya ya wadau wa kemikali.

6.3 Ushirikiano wa Kikanda

Tanzania iliendelea kushirikiana kikanda katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kushiriki mafunzo ya ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa za kikanda

za kiintelijensia (Regional Inteligence Gathering Course), yaliyoandaliwa na Ofisi ya Umoja wa Mataifa inayoshughulikia Dawa za Kulevya na Uhalifu (UNODC). Pia operesheni (Joint operation) na uelimishaji wa pamoja (Joint Sensitization) umefanyika ukihusisha nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Zambia.

Aidha, Mamlaka ilishiriki mafunzo yaliyoratibiwa na Trilateral Planning Cell (TPC) kwa kushirikiana na EU-ACT kwa ajili ya kujengewa uwezo katika matumizi ya vifaa vya TEHAMA na kielektroniki kwenye masuala ya sayansi jinai (Digital Forensic: IT and Electronic Devices). Vilevile ilishiriki mkutano wa Tume ya Kupambana na Dawa za Kulevya kwa nchi zilizo Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESACD) kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika udhibiti wa dawa za kulevya aina ya bangi. Aidha, Mamlaka ilishiriki mkutano wa *Mozambique Channel Security Talks* ili kuimarisha udhibiti wa dawa za kulevya aina ya heroin na methamphetamine kupitia njia ya kusini (Southern Route) kutoka nchi zalishi.

6.4 Ushirikiano wa Kimataifa

Tanzania imeendelea kushirikiana na mataifa mbalimbali katika kupambana na dawa za kulevya kwa kubadilishana taarifa za kiintelijensia, kubadilishana uzoefu wa mapambano dhidi ya dawa za kulevya, kuimarisha usalama wa mipaka pamoja na utambuzi wa mbinu mbalimbali zinazotumika kuficha na kusafirisha dawa za kulevya.

Mamlaka ilishiriki vikao na mafunzo vilivyoratibiwa na INCB kuhusu udhibiti wa dawa mpya za kulevya na kemikali bashirifu, ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia na udhibiti wa dawa za kulevya kupitia kampuni za usafirishaji vifurushi pamoja na udhibiti wa vifaa vya maabara vinavyoweza kutumika kutengeneza dawa za kulevya. Aidha, Mamlaka ilishiriki mkutano wa Tume ya Kimataifa ya Kudhibiti Dawa za Kulevya (Commission for Narcotic Drugs- CND) uliyofanyika nchini Austria.

Vilevile, Mamlaka ilishiriki mafunzo juu ya ukusanyaji wa taarifa za kiintelijensia kuhusu dawa za kulevya (Open Source Intelligence) yaliyoandaliwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linalojihusisha na Dawa za Kulevya pamoja na Uhalifu (United Nations Office on Drugs and Crimes – UNODC). Aidha, Mamlaka ilishiriki mafunzo ya udhibiti wa kemikali bashirifu, dawa za kulevya za viwandani na intelijensia, yaliyoratibiwa na taasisi ya kudhibiti dawa za kulevya ya Marekani (DEA).

SURA YA SABA

CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA BAADAYE

7.1 Utangulizi

Katika kipindi cha mwaka 2025 mafanikio makubwa yaliyopatikana yametokana na uwezeshaji mkubwa uliofanywa na Serikali pamoja na utashi wa kisiasa. Pamoja na mafanikio makubwa yaliyopatikana zipo changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya kupambana na dawa za kulevya nchini. Changamoto na mikakati imeainishwa kama ifuatavyo; -

7.2 Changamoto

Zifuatazo ni changamoto zinazokabili udhibiti na mapambano dhidi ya dawa za kulevya Nchini: -

i. Uelewa mdogo wa jamii juu ya tatizo la dawa za kulevya kama vile watoa huduma za afya, na viongozi ngazi za jamii.
ii. Mabadiliko ya teknolojia inayotumika katika biashara ya dawa za kulevya ikihusisha matumizi ya mitandao ya kijamii, vifaa vya kisasa kama ndege isiyokuwa na rubani, mitandao ya siri na fedha za kidijitali;
iii. Uhaba wa Vitendea kazi vya kisasa katika kukabiliana na tatizo la dawa za kulevya;
iv. Kuibuka kwa dawa mpya za kulevya (NPS) na kemikali bashirifu ambazo hazipo katika Sheria za Udhibiti wa Kitaifa na Kimataifa;
v. Kukosa ushirikiano kutoka kwa baadhi ya mashahidi;

7.3 Mikakati ya Baadaye

Mikakati ya kukabiliana na changamoto zilizoainishwa ni: -

i. Kuongeza wigo wa utoaji elimu kwa kushirikiana na wadau ili kuifikia jamii;
ii. Kuendelea kuwajengea uwezo wadau wanaoshiriki katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya ili kuongeza ufanisi katika udhibiti wa dawa hizo;
iii. Kuendelea kuboresha Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya;
iv. Kuimarisha ushirikiano na mamlaka nyingine za udhibiti ndani na nje ya nchi pamoja na wadau wote kwa ujumla.

VIAMBATA

Kiambata Na. I

Orodha ya Asasi zilizotoa Elimu kwa Mwaka 2025

Na.	Jina la Asasi
1.	Action Plan Organization
2.	Akili Platform Tanzania
3.	Alliance for Youth Advancement (AFYA)
4.	Alpha Visible Community Development
5.	Amani Sports Academy
6.	Anti-Alcoholism and Drug Addiction Organization (AADAO)
7.	Bahibo Mental Health Organization (BMHO)
8.	Bariadi Roots and Shoots
9.	Blue Cross Tanzania
10.	Bora Imani Children and Youth Foundation (BICYF)
11.	Bright House of Change Organization
12.	Bright Vision Reform Tanzania
13.	Bukoba Anti-Drugs Intellectually Organization (BAIO)
14.	City Centre Soccer Club
15.	Community on Mental Wellbeing in Tanzania
16.	Community Peers for Health and Environment Organization (CPHEO)
17.	De pores Memorial Foundation
18.	Drug Abuse and Recovery Organization (DARO)
19.	Drug Abuse Prevention Initiatives Supporting Organization in Tanzania (DAPISOITA)
20.	Empower Care Foundation
21.	Foundation for Community Involvement (FCI)
22.	Foundation for Legal and Health Support
23.	Gift of Hope Foundation
24.	Green Hope Organization

Na.	Jina la Asasi
25.	Hope Community Reviver (HCR)
26.	Jipe Moyo Centre
27.	Juza Waste Pickers Initiative
28.	Kibao Salama Foundation (KISAFO)
29.	Kibwena Community Development
30.	Kigoma Vijana Development Alliance (KIVIDEA)
31.	Kirumba Movement for Harm Reduction
32.	Konga Halmashauri Tabora
33.	Life and Hope Rehabilitation Organization
34.	Lindi Support Agency for Welfare (LISAWE)
35.	Lishe na Maendeleo Tanzania (LIMATA)
36.	Mapambano ya UKIMWI na Kifua Kikuu Temeke (MUKIKUTE)
37.	Marafiki wa Elimu Geita
38.	Methadone Family Against Drug Abuse (MEFADA)
39.	Methadone Recovery Community Empowerment Tanzania (MRCE-Tanzania)
40.	Morogoro Saving the Poor Organization (MOSAPORG)
41.	Naweza Tena
42.	Nazareth Kwaya
43.	Next Generation Keepers (NGK)
44.	Ngao ya Jamii
45.	Nugget Development in Tanzania
46.	Organization of Youth Against Risk Behaviors (OYARB)
47.	People with Drug Dependence Relief Foundation (PEDDEREF)
48.	Purple Heaven Foundation
49.	Recovery Youth with Vision (REYOVI)
50.	Rondo Women's Development Organization
51.	Rukwa Association of Non-Governmental Organization (RANGO)
52.	Saiko Senta
53.	Secure Your Life Benefit against Drug Addiction

Na.	Jina la Asasi
54.	Soma kwa Furaha Initiative (SKFI)
55.	Steps Tanzania
56.	Tanga Recovery Community
57.	Tanzania Albinism Society
58.	Tanzania Community Empowerment Organization (TCEO)
59.	Tanzania Drug Prevention Network (TDPN)
60.	Tanzania International Organization of Good Templars (T-IOGT)
61.	Tanzania Organization of Good Templars (TOGT)
62.	Tanzania Social Foundation for a Drug Free Generation
63.	Teen's Challenge
64.	Voice of Encouragement Tanzania (VET)
65.	Wounded Healer's Organization
66.	Youth Achievement Village in Tanzania (YAVT)
67.	Youth and Community Rehabilitation (YCR)
68.	Youth Community Capacity Empowerment (YOCOCE)
69.	Youth Counseling and Rehabilitation Foundation (YCRF)
70.	Youth Empowerment and Psychotherapy Aid Organization (YEPAO)
71.	Youth Empowerment Society
72.	Youth Help Home Tanzania (YOHEHOTA)
73.	Youth Relief Foundation
74.	Youth Volunteers Against Risk Behaviors (YOVARIBE)
75.	Youth Wings

Kiambata na. II

Idadi ya Watu Wenye Uraibu waliohudumiwa kwenye Nyumba za Upataji Nafuu (Sober House) kwa mwaka 2025

Na.	Jina la Nyumba	Jinsi		Mkoa
		Me	Ke	
1.	Arusha Recovery Sober House	102	0	Arusha
2.	Arusha Women Recovery Sober House	0	91	
3.	Olmotonyi Recovery House	85	0	
4.	Meru Recovery House	101	0	
5.	Njiro Recovery Sober House	205	0	
6.	Njiro Recovery Sober House	91	0	
7.	Njiro Women Sober House	0	101	
8.	Usa River Recovery Sober House	103	0	
9.	Surrender for Freedom Treatment Centre	144	0	
10.	Moshono Foundation Sober House	105	0	
11.	Northern Hill Sober House	206	0	
12.	New Life Sober House	70	0	
13.	Tasor Sober House	84	0	
14.	Zayn Hope House	40	0	
15.	Vision of Hope Sober House	30	0	
16.	Changamoto ni Matumaini	95	0	Dar es Salaam
17.	Drug Abuse Prevention Organization (DAPO)	145	0	
18.	Drug Abuse Prevention Organization (DAPO) Women	0	45	
19.	The Right Way Recovery House	91	0	
20.	The Ties That Bind Us Recovery Center	132	0	
21.	Hope again Rehabilitation and Wellness Foundation	85	0	
22.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (1)	86	0	
23.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (2)	67	0	
24.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (3)	57	0	
25.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (4)	30	0	
26.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (5)	76	0	

27.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (6)	124	0	
28.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House (7)	0	44	
29.	The Awaited Rehab Centre	20	0	
30.	Pillimissana Kisiwani Sober House na. 1	110	0	
31.	Pillimissana Kibada Sober House na. 2	61	0	
32.	Pillimissana Mikwambe Sober House na. 3	143	0	
33.	Pillimissana Gezaulole Women Sober House na. 4	0	38	
34.	Back to Life Sober House	4	0	
35.	Teen Challenge Sober House	6	0	
36.	New beginning Sober House	7	0	
37.	Utopia Addiction Sober House	3	0	
38.	Iringa Sober House	0	0	Iringa
39.	Free at Last Sober House	30	0	Morogoro
40.	Cornerstone Recovery	18	0	
41.	MRC Tanzania Kigamboni Sober House	28	0	Dodoma
42.	MRC Dodoma Sober House na. 2	25	0	
43.	Faith Community Rehabilitation Foundation	11	0	
44.	Yahwe Restoration Centre	10	0	
45.	New Vision of Life Society Sober House	81	0	Pwani
46.	Life and Hope Sober House	143	0	
47.	Women’s Hope Rehabilitation	0	30	
48.	Eso Mapinga Sober House	38	0	
49.	Bagamoyo Sober House	46	0	
50.	Mama and Papa’z Sober House	47	0	
51.	Pillimissanah Foundation	102	0	Mwanza
52.	Mwanza Sober House	38	0	
53.	Life and Hope Sober House	35	0	
54.	Teen Challenge Sober House	8	0	
55.	Lake Zone Sober House	51	0	
56.	Sobriety Forever Rehabilitation Centre	8	0	Kagera
57.	MRC Mbeya Sober House	64	0	Mbeya
58.	Simama Tena Sober House	18	0	Shinyanga
59.	MRC Kahama Sober House	29	0	

60.	Kilimanjaro Recovery Home	20	0	Kilimanjaro
61.	Surrender for Freedom Treatment Centre	72	0	
62.	Serenity Gate Rehab (SGR)	60	0	
63.	Kilimanjaro New Vision and Sobriety 1	79	0	
64.	Kilimanjaro New Vision and Sobriety 2 (Women)	0	23	
65.	Brother of Good Shepherd	14	0	
66.	Helping Hand Foundation	41	0	
67.	Faith Addiction Recovery Centre	17	0	
68.	Courage on Recovery Foundation	52	0	Tanga
69.	Gift of Hope Foundation	62	0	
70.	Tanga Drug Free Sober House	73	0	
71.	Gate Away Sober House	26	6	
72.	MRC Tunduma Sober House	19	0	Songwe
	Jumla	**4,073**	**378**	
	Jumla kuu	**4,451**		

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya,
S.L.P 80327, 8 Barabara ya Kivukoni,
11486 Dar es Salaam Barua pepe: cg@dcea.go.tz
Tovuti: www.dcea.go.tz Instagram: @dceatanzania
Twitter: @dceatanzania Facebook: dcea_tz
YouTube: DCEATV Simu ya bure: 119